SportPesa
TZS. 846,297,200
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mwanafunzi** UDSM ajirusha ghorofani na kufariki dunia

UKURASA 3



VILLA YAKAMILISHA USAJILI WA COUTINHO

UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Januari 13, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580824

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Chenge akoleza moto kinyang'anyiro uspika

● **Ajitosa** kupambana na Dk. Tulia, Zungu, wanaowania CCM wafikia 30... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MWANDISHI IPP ASHINDA TUZO YA AFYA KIMATAIFA**



SHIRIKA la Merck Foundation la Ujerumani kwa kushirikiana na wake wa marais wa Afrika, limemtangaza mwandishi wa habari wa magazeti ya...

## Sherehe za miaka 58 ya Mapinduzi Zanzibar zafana

UKURASA 3



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk.Hussein Ali Mwinyi, akikagua gwaride la vikosi vya ulinzi na usalama, baada ya kupokea salamu ya heshima wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Miaka 58 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika Uwanja wa Amaan jana. **Picha zaidi Uk. 18. PICHA: IKULU**



Majeneza yenye miili ya waandishi wa habari waliofariki katika ajali ya gari, wakati wa kutoa heshima za mwisho katika Uwanja wa Nyamagana, jijini Mwanza jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

## Nape aongoza mamia kuaga miili ya waandishi

UKURASA 2

**MICHEZO** FAINALI YA MBINU, AKILI UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Mwandishi IPP ashinda tuzo ya afya kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Merck Foundation la Ujerumani kwa kushirikiana na wake wa marais wa Afrika, limemtangaza mwandishi wa habari wa magazeti ya The Guardian na Nipashe, Christina Mwakangale, kuwa mshindi wa kwanza wa Tuzo ya Afya ya Uzazi Mwaka 2021 kwa nchi za Afrika Mashariki.

Mbali na Mwakangale, Watanzania wengine walioshinda nafasi ya kwanza kwenye tuzo hiyo mtandaoni ni Veronica Mrema, kutoka blog ya matukio na maisha pamoja na Adam Gabriel Hhando, wa CG FM , kipengele cha redio.

Shirika hilo lilitangaza kuanza kwa mashindano hayo mwaka jana na kushirikisha nchi tofauti barani Afrika kutoka kanda mbalimbali kuwania tuzo kwa waandishi wa habari kutoka nchi za Kusini mwa Afrika; Afrika Mashariki; Afrika Magharibi na zinazozungumza lugha ya Kifaransa.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Seneta Dk. Rasha Kelej, akitangaza majina ya washindi hao kwenye taarifa yake jana, alisema lengo la mashindano hayo ni kukuza uelewa na kutoa elimu kwa jamii kuachana na dhana potofu dhidi ya watu waliokosa watoto, wakiwamo wagumba na tasa. Mkurugenzi huyo ambaye pia ni rais wa shirika hilo linaloshirikiana na wake wa marais wa barani Afrika, alisema tuzo hizo hutolewa kila mwaka kwa kuhusisha waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali vya habari.

"Kaulimbiu ya tuzo hizo ilikuwa kukuza uelewa kuhusu kinga ya ugumba, kuvunja unyanyapaa na kuwawezesha wasichana na wanawake kupata elimu. Ninayo furaha kuwatangaza washindi hawa wa Merck Foundation Africa Media Recognition Awards 'More Than a Mother' 2021.

"Pia nachukua fursa hii kuwashukuru marais wa Afrika kwa nia yao thabiti na kushirikiana na shirika kama mabalozi wa Merck Foundation Zaidi ya Mama. Ninapongeza vyombo vya habari barani Afrika ambavyo vimekuwa sauti ya wasio na sauti na kuongeza uelewa kwenye jamii hususan unyanyapaa kwa wagumba, tasa na wanaopitia changamoto za kupata watoto," alisema Dk. Kelej.

Pia alibainisha kwamba kila mara jukumu kuu la vyombo vya habari vina uwezo wa kuleta mabadiliko ya kitamaduni katika jamii zetu kwa njia ya gharama nafuu.

"Ninawakaribisha washindi wote kuwa wanachama wa walimu wetu wa Merck Foundation na kufanya kazi kwa karibu nasi, ili kuunga mkono, kuwawezesha wanawake na wasichana katika ngazi zote.

"Nimefurahishwa sana na kazi iliyoonyeshwa na washindi wetu wote; kwa hivyo inanipa furaha kubwa kutangaza kwamba Merck Foundation pia inawazawadia washindi kwa kuwapa ufikiaji wa mwaka mmoja wa programu ya MasterClass," alisema.

Alisema kozi hiyo itawajengea washindi hao uzoefu wa kipekee wa mtandaoni na kujifunza ya haraka ambayo hufikiwa popote kwa njia ya mtandao.

"Ningependa pia kutoa wito wa Maombi kwa Merck Foundation Africa Media Recognition Awards 'Zaidi ya Mama' kwa mwaka 2022."

# Chenge akoleza moto kinyang'anyiro uspika

**Na Waandishi Wetu**

MOTO umekolea kinyang'anyiro cha kuwania nafasi ya Spika wa Bunge ndani ya CCM. Hivyo ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na watu mashuhuri kujitosa katika kuwania nafasi hiyo iliyoachwa na Job Ndugai baada ya kujiuzulu.

Jana, mwanasheria nguli nchini, Andrew Chenge, jana alijitosa kuwania nafasi hiyo kwa kuchukua fomu hivyo kufanya walioonyesha nia na kuingia ulingoni kwa kuchukua fomu kufikia 30.

Kuingia kwa mwanasheria huyo na mwanasiasa maarufu, kumeongeza joto la kinyang'anyiro kutokana na nafasi yake pamoja na nyadhifa ambazo amewahi kuzishika serikalini.

Chenge ambaye hadi mwaka 2015 alikuwa Mbunge wa Bariadi, aliwahi kuwa mwanasheria mkuu wa serikali kuanzia mwaka 1993 hadi 2005. Pia aliwahi kuwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na ile ya Miundombinu (sasa Ujenzi na Uchukuzi). Nafasi nyingine aliyowahi kushika ni mwenyekiti wa Bunge.

Aidha, kuingia kwa kigogo huyo kunafanya mchuano kwa dhahania kuonekana mkali kwa sababu wako watu mashuhuri wengine ambao wamejitosa akiwamo Naibu Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini Dodoma katika Ofisi ya Makao Makuu ya CCM, Katibu Msaidizi Mkuu, Idara ya Oganaizesheni, Solomon Itunda, alisema kwa siku ya jana pekee wanachama 13 walijitokeza kuchukua fomu, akiwamo Chenge.

Itunda alisema kwa siku ya jana katika ofisi ya makao makuu, waliochukua fomu ni Dk. Mussa Shaffi Ngonyani, Faraji Rushagama, Hamisi Rajabu, Dk. Titus Mlengeya Kamani na Asia Juma Abdallah.

Alisema katika kituo cha ofisi ndogo ya Lumumba jijini Dar es Salaam waliochukua fomu ni Festo John Kipate, George Francis Nangale, Barua Abdi Mwakilanga, Zahoro Rashid Hanuna, Chenge, Thomas Kirumbuyo pamoja na Angelina Belo John.

Kadhalika, alisema katika kituo cha Ofisi Kuu ya Zanzibar kwa mara ya kwanza amejitokea mwanachama mmoja aliyechukua fomu ambaye ni Mhandisi Abdul Azizi Jaad Hussein.

Kazi ya kutoa fomu za kugombea nafasi ya Spika wa Bunge la Tanzania ndani ya CCM zilianza rasmi Januari 10, mwaka huu, baada ya Ndugai kutangaza kujiuzulu Januari, 6 mwaka huu. Uchukuaji huo unatarajia kufungwa keshokutwa.

Tangu kutangazwa kwa mchakato huo siku ya kwanza wanachama tisa walijitokeza kuchukua fomu, siku ya pili walijitokeza wanachama wanane na jana wanachama 13.

■ **Imeandaliwa na Paul Mabeja (Dodoma), Elizabeth Zaya (Dar)**



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa na aliyekuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Job Ndugai baada ya mazungumzo, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Nape aongoza mamia kuaga miili ya waandishi

**Na Anthony Gervas,**
MWANZA

MAMIA ya wakazi wa Jiji la Mwanza, wakiongozwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, jana walifurika katika Uwanja wa Nyamagana kuaga miili ya wapendwa wao waandishi wa habari waliofariki dunia juzi katika ajali ya gari wakiwa kwenye safari ya kikazi.

Akiongoza kuaga miili hiyo, Waziri Nnauye alisema ni pigo kubwa lililotikisa taifa.

Miili ya waandishi hao, akiwamo dereva Paul Silenge, aliyekuwa akiwaendesha waandishi hao ni kati ya watu 14 waliopoteza maisha katika ajali iliyotokea juzi ya kugongana uso kwa uso na gari la abiria Toyota Hiace, wakati wakielekea wilayani Ukerewe kikazi.

Nnauye alisema msiba huo umetikisa Kanda ya Ziwa na Taifa kwa ujumla, wakiwamo watu wanane waliokuwa katika gari hilo la abiria.

Ajali hiyo ilitokea wakati wanahabari hao wakiwa katika msafara wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, wakielekea wilayani Ukerewe kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao kikazi.

Alisema waandishi waliofariki dunia ni mashujaa na wamekutwa na ajali hiyo wakiwa kazini na kwamba watakumbukwa daima na Watanzania na Wanamwanza wote kwa ushirikiano wao wa kazi na serikali na kutoa pole kwa familia zilizopatwa na msiba huo.

"Nimeteuliwa katika wizara hii na Rais Samia Suluhu Hassan siku chache, nimeanza kazi na pigo, hawa waandishi wa habari ni mashujaa ambao watakumbukwa daima kwa mchango wao walioutoa katika tasnia ya habari," alisema Nnauye.

Alisema, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa pia ametuma salamu za rambirambi kwenye familia za wafiwa na waandishi wa habari wa Mkoa wa Mwanza.

Katika hotuba yake Nnauye alisema atahakikisha anasimamia uhuru wa vyombo vya habari, sheria gandamizi na haki zao kupitia wizara yake ili kuifanya taaluma ya habari iheshimike.

Waandishi wa habari waliofariki dunia kwa ajali hiyo ni Husna Mlanzi (ITV), Anthony Chuwa (Daily News), Johari Shani (Pembezoni TV), Ofisa habari Mkoa wa Mwanza, Abely Ngapemba pamoja na Ofisa Habari Wilaya ya Ukerewe, Stephen Msengi.

Katika ajali hiyo waandishi wawili waliojeruhiwa na kulazwa katika Hospitali ya Kanda Bugando kwa matibabu zaidi ni Tunu Herman pamoja na Elias Vanny na majeruhi sita waliokuwa kwenye Hiace, lililokuwa likielekea Mwanza.

Mamia ya wananchi, ndugu na jamaa na waandishi wa habari, walifurika uwanja wa Nyamagana kuaga miili ya wapendwa wao kabla ya kusafirishwa kwa maziko katika mikoa yao. Marehemu Husna Mlanzi, alizikwa jijini Mwanza.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alisema sio ajabu waandishi hao kuwaita mashujaa kutokana na kupata ajali hiyo wakiwa kazini kushirikiana na serikali kutangaza mema ya mkoa wake wakitumia kalamu zao.

Gabriel alisema kila mtu atapitia njia ya mauti na siku zikifika hazikwepeki, lakini msiba huo umemtikisa. Mkuu huyo alilazimika kuhubiri injili kwa muda, akisoma maandiko matakatifu yanayosema maisha ni zawadi kwa kila binadamu aliyepo chini ya jua.

## HABARI KITAIFA

# Sherehe miaka 58 Mapinduzi zafana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHEREHE za miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar zilifikia kilele chake jana kwa kupambwa na kila aina ya shamra shamra zilizofana na kuhudhuriwa na umati wa wananchi na wageni kutoka nje ya Zanzibar.

Nderemo na vifijo zilitawala katika Uwanja wa Amani Mjini baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuwasili uwanjani hapo majira ya saa 3:20 asubuhi akiwa katika gari la wazi maalumu na kuwalaki wananchi waliofika viwanjani hapo.

Mizinga 21 ikapigwa na vikosi vya ulinzi na usalama na baadaye kupokea maandamano ya wananchi wa mikoa mitano ya Zanzibar wakiwamo waliovalia sare za Chama cha ACT-Wazalendo na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Pia, Dk. Mwinyi alikagua na kupokea gwaride kutoka kwa askari wa vikosi vya ulinzi na usalama vilivyopita mbele yake kwa mwendo wa pole na haraka na kutoa heshima.

Gwaride hilo pia lilitoa salamu ya utii na wimbo wa taifa wa Zanzibar na wimbo maalumu wa ukombozi na kuwaenzi mashujaa.

Makamanda wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), walipita uwanjani hapo mbele ya rais wakiwa na zana zao za kivita.

Burudani za ngoma za utamaduni zilitumbuiza kuwaburudisha viongozi mbalimbali wa kitaifa akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Marais wastaafu Amani Karume, Dk. Ali Mohamed Shein na Dk. Jakaya Kikwete.

Wengine waliohudhuria sherehe hizo ni mawaziri wakuu wastaafu akiwamo Frederick Sumaye, Makamu wa Rais mstaafu Dk. Muhamed Gharib Bilali, Makamu wa Pili wa Rais Hemed Abdullah, Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, mjane wa Rais wa kwanza wa Zanzibar, Fatma Karume na mawaziri wa SMT na SMZ.

Akitoa neno la shukran, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Abdullah, alimpongeza Rais Samia na viongozi wote kushiriki kuzindua miradi katika shamrashamra za Mapinduzi.

"Kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar tunakushukuru na kukupongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi kwa hotuba nzuri uliyoitoa jana kwa vyombo vya habari na umejenga matumaini makubwa kuendeleo katika maendeleo tunayotarajia na tutaendelea kukuunga mkono," alisema.

Aliwapongeza wananchi kwa kuzinga mkono serikali zote mbili za SMT na SMZ na marais wanavyoiongoza nchi kwa uchapakazi wao.

# Mwanafunzi UDSM ajirusha ghorofani na kufariki dunia

**Na Maulid Mmbaga**

MWANAFUNZI wa mwaka wa pili anayesomea Shahada ya Uhasibu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Manawa Horera (22), amefariki dunia kwa kujirusha kutoka ghorofani katika Hosteli za Magufuli zilizoko chuoni hapo.

Taarifa zinaeleza kwamba Horera alijirusha kutoka ghorofani muda mfupi baada ya kutuhumiwa kuiba kompyuta mpakato (Laptop) iliyokuwa katika chumba cha mwanafunzi mwenzake.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa lilitokea Januari 11 mwaka huu saa 8:30 usiku katika hosteli hizo zilizoko eneo la Ubungo mkoani Dar es Salaam.

Kamanda Muliro alisema mwanafunzi huyo aliingia kwenye chumba cha mwanafunzi mwenzake aliyejulikana kwa jina la Hamza Abdulhaman na kutuhumiwa kuiba Laptop aina ya HP.

Kamanda Muliro alisema: "Baada ya mwanafunzi huyo kubainì kuwa ameonekana na wanafunzi wenzake aliamua kuruka kupitia dirishani akitaka kukimbia kutoka ghorofa ya pili kilipo chumba hicho na kudondoka mpaka chini na kusababisha kuumia maeneo mbalimbali ya mwili wake."

Alisema baada ya kupata majeraha, Horera alikimbizwa katika hospitali ya chuo na baadaye alipelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) lakini hali ilibainika kuwa ameshapoteza maisha.

Aliongeza kuwa kumekuwa na taarifa kutoka katika hosteli wanazoishi wanafunzi hao kuwapo na matukio ya wizi hususani ya kuibiana vitu kama Laptop akibainisha kwamba matukio hayo yanafanywa na wanafunzi wenyewe.

Aidha, alieleza kuwa katika uchunguzi uliofanywa na Jeshi la Polisi umeonyesha baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya jinai, ikiwamo wizi, akidai kuwa hali hiyo inaweza kukatisha ndoto za mwanafunzi katika masomo yake.

Kamanda Murilo alisema: "Vitendo hivyo ni vya kijinai na mtuhumiwa anaweza kufikishwa mahakamani, Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wanafunzi wote kuacha kujihusisha na vitendo vya kihalifu kwani vinaweza kuharibu ndoto zao."


**SAMBA SERVICE COMPANY LIMITED**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA SIKU YA JUMANNE TAREHE 18/01/2022**

Kwa idhini niliyopewa na Baraza la ARDHI na NYUMBA la Bukoba, kutokana na kesi Na. 01/2016 Kampuni ya Samba itauza kwa mnada wa Hadhara nyumba iliyopo Kitongoji Mishenye Kijiji Bukabuye mali ya Gustodes Gerazi ili kulipa deni analodaiwa na Justodes Mugisha na Sauda Issack. Mnada utaanza saa sita mchana.

Pia kampuni ya Samba itauza nyumba mali ya Selina Peter iliyopo mtaa wa Magoti kata Kibeta, ili kulipa fedha anayodaiwa na Denis Mutashobya kutokana na kesi ya madai Na. 86/2019. Mnada utaanza saa nne Asubuhi. Hivyo Wananchi wote mnaombwa kuwahi mapema kukagua nyumba kabla ya mnada kuanza.

**MASHARTI YA MNADA**

Mnunuzi atalazimika kulipa asilimia 25 za kiwango kitakachofikiwa na asilimia 75 zilipwe ndani ya siku 14. Endapo mnunuzi atashindwa kukamilisha malipo yote ndani ya muda, asilimia 25 hazitarejeshwa na mnada utafanyika upya.

**Imetolewa na AZATH J. SIMBA**

..................................

**DALALI WA MAHAKAMA (M) KAGERA**



Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

## PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

**PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER PROTECTION 2019.**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | |
| a) Monthly | FREE | FREE |
| b) Interm | TZS 4,300.00 | $ 5.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | FREE | Up to 5000 FREE |
| | | Above 5000 0.26% |
| 5. Cash Deposit Charges | FREE | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | TZS 12,800.00 | $ 6.00 |
| 7. A/c Closure charges | TZS 12,800.00 | $ 13.00 |
| 8. Activation of Dormat A/c | TZS 5,100.00 | $ 6.00 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly | TZS 4,300.00 | $ 5.00 |
| b) Interm | Fixed TZS 4,300.00 | Fixed $5.00 |
| | plus For each page TZS 500.00 | For each page $1.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MILLION FREE | Upto 5000 FREE |
| | ABOVE 25 MILLION 0.11% | 5000 to 10,000 - 0.26% |
| | | Above 10,000 0.43% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO FREE | Upto 10,000 FREE |
| | ABOVE 50 Million 0.11% | > 10,000- 0.26% |
| 5. Balance Confirmation certificate | TZS 21,200.00 | $13.00 |
| 6. Stop Payment Charges | TZS 25,500.00 | $13.00 |
| 7. Cheque Clearing Charges | | |
| a) Inward | TZS 1,300.00 | $1.00 |
| b) Outward | FREE | FREE |
| 8. Cheque Return Charges | | |
| a) Inward | TZS 25,500.00 | $13.00 |
| b) Outward | TZS 25,500.00 | $13.00 |
| 9. A/c closure charges | TZS 21,200.00 | $17.00 |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | |
| **1. Cash Withdrawal** | | |
| Upto 100,000 | TZS 1,700.00 | NA |
| 101,000 to 200,000 | TZS 2,600.00 | NA |
| 201,000 to 400,000 | TZS 4,300.00 | NA |
| 401,000 to 600,000 | TZS 5,100.00 | NA |
| 601,000 to 999,000 | TZS 6,800.00 | NA |
| **2. Funds Transfer/Mobile Wallet** | | |
| Upto 100,000 | TZS 500.00 | NA |
| 101,000 to 250,000 | TZS 900.00 | NA |
| 251,000 to 500,000 | TZS 1,700.00 | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | TZS 4,300.00 | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | TZS 8,500.00 | NA |
| **Mobile Banking Services** | | |
| A) Monthly Subscription Charges | TZS 500.00 | NA |
| B) PIN Request | TZS 2,200.00 | NA |
| **D. LOCKERS RENT YEARLY** | | |
| 1.SMALL | TZS 296,700.00 | NA |
| 2. MEDIUM | TZS 508,500.00 | NA |
| 3. BIG | TZS 635,600.00 | NA |

| E. REMITTANCES | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. TISS | TZS 8,450.00 | EQUIVALLENT TO TZS 8450 |
| **2. E Remittances** | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | TZS 17,000.00 | $ 9.00 |
| 1001 to 5000 | TZS 20,400.00 | $ 11.00 |
| 5001 to 10000 | TZS 40,700.00 | $ 22.00 |
| 10,001 and above | TZS 84,800.00 | $ 43.00 |
| **3. SWIFT** | | |
| **a) Swift Outward** | | |
| Upto 5,000 | NA | $ 39.00 |
| 5,001 to 10,000 | NA | $ 51.00 |
| above 10,000 | NA | $ 77.00 |
| **b) Swift Inward** | | |
| Upto 5,000 | NA | $ 11.00 |
| 5,001 to 10,000 | NA | $ 16.00 |
| above 10,000 | NA | $ 26.00 |

| F. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - TZS 21,200.00 | Upto 5,000 - $85.00 |
| | 5Mio to 10 Mio - TZS 169,500.00 | 5000 to 10,000 - $170.00 |
| | 10 Mio to 25mio - TZS 339,000.00 | Upto 20,000 - $255.00 |
| | 25 mn to 500 mio - 1.28% | 20,000 to 500,000 - 1.28% |
| | >500mio--* (*minimum 7.5mio) 1.06% | >500,000--* (*minimum 7,500) 1.06% |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 MILLION FREE | Upto 50,000 FREE |
| | >100 Mio (-Min 300,000) 0.26% | >50,000 - (Min 150) 0.26% |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - TZS 21,200.00 | Upto 20,000 - $255.00 |
| | 5 Mio to 10 Mio - TZS 169,500.00 | 20,000 to 500,000 - 1.53% |
| | 10Mio 25mio - TZS 381,400.00 | >500,000--* (*minimum 9000) 1.28% |
| | 25 mn to 500 mio - 1.53% | |
| | >500mio--* (*minimum 9mio) 1.28% | |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio - TZS 21,200.00 | Upto 50,000 $22.00 |
| | >100 mio - TZS 42,400.00 | >50,000 $43.00 |
| 5.Credit Reference Report Charges from D&B Tanzania | TZS TZS 101,700.00 | $43.00 |
| 6.Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders 1.70% | of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders 1.70% |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | |
| Bonds & Guarantees | ( Min TZS 75,000) 1.02% | 1.02% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) 0.43% | 0.43% |

| H. LETTER OF CREDIT | TZS | USD |
|---|---|---|
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | |
| Opening commission | NA | ( Min $ 200) |
| LC amendment Commission | NA | ( Min $50 max 350) 1.02% |
| Swift charge for LC opening | NA | 0.34% |
| Swift charge for other message/amendments | NA | $34.00 |
| Extensions - Commissions | NA | ( Min $200) $34.00 |
| LC cancellation charges | NA | ( Min $200) 1.02% |
| Non payment of Bills on due date | NA | Till Payment 1.02% |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | |
| Advising commission | NA | $119.00 |
| Confirmation Commission | NA | ( Min $150) 0.43% |
| Negotiating bills under LC | NA | (Min $75+cuourier+int) 0.43% |
| Reimbursement claim paid | NA | ( Min$75) 0.43% |
| Extensions - Commissions | NA | ( Min $200) 1.02% |
| Collection of Export LC | NA | (Min $75+cuourier+int) 0.43% |
| Amendments | NA | $64.00 |

**OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |

**i. Fixed Deposits of TZS**

| Amount in TZS | up to TZS 50 Million | Over TZS 50 Million | Above 100 Million |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 3.50% | 4.50% | 5.50% |
| 91-180days | 4.50% | 5.50% | 6.50% |
| 181-364 days | 5.50% | 7.00% | 7.50% |
| Above 1 year | 8.00% | 8.25% | 8.50% |

**ii. Fixed Deposits of USD**

| Amount in USD | up to USD 50,000 | Over USD 50,000 | Over USD 100,000 |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 91-180days | 2.00% | 2.75% | 3.25% |
| 181-364 days | 2.50% | 3.00% | 3.50% |
| Above 1 year | 3.00% | 3.50% | 4.00% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| JOHN CHARLES | GM-OPERATIONS | SIGNED | 10-01-2022 |
| SALMA MRISHO | HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE | SIGNED | 10-01-2022 |
| KAUSHENDRA TIWARI | GM-CREDIT | SIGNED | 10-01-2022 |

# Mkopo wa tril. 7/-BADEA wanukia

**Na Benny Mwaipaja,**
DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amefanya mazungunzo kwa njia ya mtandao na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (BADEA), Dk. Sidi Ould Tah.

Katika mazungumzo hayo, walijadili namna ya kuharakisha upatikanaji wa fedha za mkopo nafuu na msaada unaokadiriwa kufikia dola za Marekani bilioni tatu sawa na takriban Sh. trilioni saba zitakazotolewa na benki hiyo katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango jana ilisema mkutano huo uliwahusisha pia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Jamal Kassim Ali; Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega.

Akizungumza katika mkutano huo, Dk. Nchemba alisema serikali imeazimia kuuelekeza mkopo huo kwenye miradi 32 iliyoko Tanzania Bara na Visiwani katika sekta mbalimbali zikiwamo kilimo cha umwagiliaji, mifugo, upanuzi wa miundombinu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na uwezeshaji wa serikali za mitaa.

Dk. Nchemba alibainisha kuwa pamoja na uwekezaji wa fedha hizo katika miradi ya kimkakati itakayosaidia kukuza ajira na kuharakisha ukuaji wa uchumi wa nchi, mkopo na misaada hiyo utasaidia kuendeleza sekta binafsi kwa njia ya ukuzaji biashara ya uagizaji kwa sekta binafsi na usafirishaji wa bidhaa kwa taasisi za kifedha nchini. Aliwaagiza wataalamu mbalimbali wa serikali ikiwamo Wizara ya Kilimo kuainisha sehemu ya eneo la hekta milioni 29 linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kuwa na maandiko ya kitaalamu yanayohusu maeneo hayo ili yapatiwe fedha.

Naye Waziri Bashe alisema fedha kutoka BADEA zitasaidia kuendeleza miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kwenye miradi 19, ili kuongeza tija katika eneo la umwagiliaji linalokadiriwa kufikia hekta milioni 1.2 kati ya hekta milioni 29 zilizoko sasa.

Dk. Tah alisema benki yake imejipanga kutoa kiasi hicho cha fedha cha dola za Marekani bilioni tatu na kwamba atatuma timu ya wataalamu kutoka benki hiyo kufika nchini na kuungana na wataalamu wa ndani itakayoungana na timu ya wataalamu wa ndani kujadili kwa kina zaidi namna ya kutekeleza mpango huo.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akishiriki katika mkutano wa dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), jijini Lilongwe, nchini Malawi jana. PICHA: OMR

# Bashe: Mimi na Mkenda tulijenga misingi imara maendeleo ya kilimo

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Kilimo Hussein Bashe, amesema katika kipindi cha mwaka mmoja alichofanya kazi na Prof. Aldof Mkenda, wamejenga misingi mizuri ambayo ataendelea kuifanyia kazi ili kuhakikisha kilimo kinasonga mbele.

Bashe alisema changamoto nyingi zinawakabili, hivyo ni lazima wazifanyie kazi na kwamba ndani ya mwaka mmoja, amepata ujuzi mkubwa kutoka kwa Prof. Mkenda na kuahidi kuyatekeleza yote.

Ili kuhakikisha waliyoyafanya yanatimia, alimwomba Prof. Mkenda ambaye sasa ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, kutoa uopendeleo lwa Wizara ya Kilimo ikiwamo kutenga fedha kwa ajili ya kusomesha wataalamu wa kilimo nje ya nchi ili wakirudi wasaidie kuendeleza sekta ya kilimo.

"Namwomba kakaangu Profesa Mkenda kulifanyia kazi suala la kusomesha wataalamu ili kuinua kilimo hapa nchini," alisema Bashe.

Juzi Waziri Mkenda alikabidhi ofisi kwa Waziri Bashe huku akiweka wazi kwamba amekabidhi kwa mtu anayejua vizuri ofisi hiyo na kazi.

Prof. Mkenda pia aliwashukuru watumishi wa wizara hiyo kwa ushirikiano waliompa alipokuwa waziri wa kilimo.

"Nakabidhi ofisi kwa mtu anayejua wizara hii maana nilipokuja hapa nilimkuta Bashe. Tumefanya kazi pamoja anaifahamu vizuri ofisi na mengi yaliyomo humu anayafahamu. Nakutakia kila la heri kwenye utumishi wako," alisema Mkenda.

"Mimi na Bashe tumefanya kazi pamoja kwa ushirikiano mkubwa. Kuna wakati mambo yalikuwa yakiwaka moto tunakutana haraka usiku ili kujadili na kutoka na msimamo mmoja," alibainisha.

Prof. Mkenda alisema sekta ya kilimo ina changamoto kubwa, lakini kwa sasa iko katika mikono salama na kuwataka waliobaki kutekeleza majukumu yao kwa weledi ili kuondoa baadhi ya vikwazo vilivyobaki.

Waziri Mkenda alkiwashukuru watumishi wa wizara hiyo kwa ushirikiano mkubwa waliompa wakati wa mchakamchaka wa utekelezaji majukumu yake.

# Mhagama aahidi kuboresha utumishi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema amedhamiria kuimarisha misingi ya utendaji kazi kwenye utumishi wa umma ili wananchi wanufaike na huduma zitolewazo na taasisi za umma.

Jenista alitoa ahadi hiyo juzi jijini Dodoma wakati wa kikao kazi na watumishi wa idara za uendelezaji sera na utawala wa utumishi wa umma.

Alisisitiza kuwa ujio wake katika ofisi hiyo, si wa kutengua torati bali ni kuendeleza mazuri yaliyofanywa na mtangulizi wake na kuweka mikakati madhubuti ya kuboresha utumishi wa umma.

"Ninaposema sijaja kutengua torati nina maana ya kuwa nimekuja kuongeza nguvu kiutendaji ili kumsaidia Rais kuboresha utumishi wa umma na kuendeleza mazuri yaliyokwishafanyika na watangulizi wangu," alisisitiza Mhagama.

Waziri Mhagama aliongeza kuwa atatumia dhamana aliyopewa na Rais kutatua changamoto zinazowakabili watumishi wa umma ili kuwa na morali ya kutoa huduma bora kwa umma.

"Tunaona imani kubwa aliyo nayo Mheshimiwa Rais kwa watumishi wa umma, hivyo nikiwa ndiye waziri mwenye dhamana ya kumsaidia kusimamia utumishi wa umma na utawala bora, nitahakikisha watumishi wa umma wanafanya kazi kwa bidii na uadilifu ili kuendana na kaulimbiu yake ya kazi iendelee," alisema.

Mhagama alisema mtumishi wa umma ana mchango mkubwa wa kutimiza ndoto ya Rais ya kuleta maendeleo kwa wananchi ndiyo maana amekuwa akiwahimiza waajiri kuwapatia watumishi wa umma stahiki zao kwa wakati ili wawe na ari kiutendaji.

Waziri Mhagama alianza vikao kazi na watumishi wa ofisi yake baada ya kuapishwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**TANGAZO**

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES

| S/N | ITEM/TRANSACTION | | |
|---|---|---|---|
| SECTION A | SAVINGS ACCOUNTS | RETAIL | CORPORATE |
| 1 | FREEDOM SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 15,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1,000 instant charge | |
| 2 | GENERAL SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| 3 | EMPLOYEE SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS15,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 USD 10 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 4 | SAVINGS ACCOUNT INDIVIDUALS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 5 | SAVINGS ACCOUNT SALARY | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 6 | SAVINGS ACCOUNT DOMICILARY | | |
| | Required minimum opening balance | USD10 | |
| | Minimum operating balance | USD 5 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1% per Transaction | |
| 7 | U-CARE CHILDREN SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | USD 15 | |
| | Minimum operating balance | USD 15 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 or its equivalent | |
| 8 | MALAIKA ACCOUNT | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | NIL | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 9 | JANJA ACCOUNT | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | NIL | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 10 | KIZAZI KIPYA ACCOUNT | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS20,000 | |
| | Minimum operating balance | NIL | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 11 | HAZINA ACCOUNT | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| SECTION B | CURRENT ACCOUNTS | | |
| 1 | INDIVIDUAL CURRENT ACCOUNT | | [illegible] |
| | Required minimum opening balance | TZS 30,000 | TZS 100,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 10,000 | TZS 100,000 |
| | Monthly maintenence fee | TZS 10,000 | TZS 12,000 |
| | Cash withdrawal at counter | 1 PER MILLE | TZS A/C 1 PER MILLE |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 5% | TZS A/C PLR + 10% |
| 2 | DIPLOMAT ACCOUNTS | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100 | N/A |
| | Minimum operating balance | USD 100 | N/A |
| | Monthly maintenence fee | NIL | N/A |
| | Cash withdrawal at counter | NIL | N/A |
| | Closing account | NIL | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | NIL | N/A |
| | Outward fund transfers(TTs) | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 | N/A |
| | Inward fund transfers(TTs Incoming) | NIL | N/A |
| | FOREX exchange | Favourable rates will be applied | N/A |
| 3 | DOMICILIARY CURRENT ACCOUNT | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Minimum operating balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Monthly maintenence fee | USD 12 or its equivalent | USD 15 or its equivalent |
| | Minimum search fees | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 |
| | Cash withdrawal | 1% per Transaction | 1% per Transaction |
| | Cheque book - 25 LEAF | USD 10 or its equivalent | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 2% | PLR + 2% |
| | Transfer From TZS to DOMICILIARY/ DOMICILIARYto TZS | NIL | NIL |
| SECTION C | DEPOSIT ACCOUNTS | | |
| 1 | Call Accounts | | Call Accounts |
| | Minimum opening balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Monthly Average balance requirement | Negotiable | Negotiable |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| 2 | Term Deposits | | Term Deposits |
| | Minimum deposit - local currency | TZS 500,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum deposit - USD | USD 1,000 | USD 10,000 or equivalent |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| SECTION D | ELECTRONIC BANKING | | |
| 1 | E-Banking | | E-Banking |
| | Internet banking monthly subscription | TZS 2,000 Per Month. | TZS 10,000 per Month |
| | Internet banking ( Re issue pin) | FREE | FREE |
| | U - Direct (Reversal of transaction) | FREE | FREE |
| | E-statement (self downloaded) | FREE | FREE |
| | POS purchase (Local) | FREE | N/A |
| | POS purchase (International) | FREE | N/A |
| | POS cash withdrawal | TZS1500 | TZS1500 |
| | ATM reversal | FREE | N/A |
| | Fund transfer/ company load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Card Load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Manual pin change | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per transaction |
| | U-MOBILE(mobile banking-Bank to wallet) | TZS 1,000 (0 - 200,000/=) and TZS 2,000 (200,001 - 400,000/=) | N/A |
| | Card to card transfer | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per tr |
| | Agency Banking Withdraw | | |
| | 1,000-9,999 | TZS500 | TZS500 |
| | 10,000-49,999 | TZS900 | TZS900 |
| | 50,000-99,999 | TZS1,200 | TZS1,200 |
| | 100,000-299,999 | TZS2,000 | TZS2,000 |
| | 300,000-499,999 | TZS3,500 | TZS3,500 |
| | 500,000-1,000,000 | TZS4,500 | TZS4,500 |
| | Uconnect Withdraw | 2% of the principle | 2% of the principle |
| | Uconnect Deposit | 1.5% of the principle | 1.5% of the principle |
| | Africash | TZS 6000 + 1.5% of the principal amount sent/USD 4.45 + 1.5% of the principle amount to be sent | N/A |
| 2 | Visa Debit Card | | N/A |
| | Issuance fees | TZS 10,000 | |
| | Re-issuance fee | TZS 10,000 | |
| 3 | Visa Perapid Cards | | N/A |
| | Issuance fees for instant card | TZS 12,000 | N/A |
| | Issuance fees for personalized card | TZS 16,000 | N/A |
| | Re-issuance fees | TZS 12,000 | N/A |
| | Online Passcode reset fee | TZS 1,500 | N/A |
| | ATM Pin reset fee | TZS 1,500 | N/A |
| | Loading fee | TZS 1,000 | N/A |
| | Online shopping fee - Local transactions | FREE | N/A |
| | Online shopping fee/Web - Int. transactions | FREE | N/A |
| 4 | ATM Withdrawals | | N/A |
| | At UBA ATMs (On us) | TZS 1000 | N/A |
| | ATM Balance inquiry(Local) | TZS 200 | N/A |
| | ATM Balance inquiry(international) | TZS 1000 | N/A |
| | To other banks ATM (On others/OFF US)Local | TZS 2,500 | N/A |
| | international ATM withdraw | TZS 6000 | N/A |
| | Umoja switch ATM withdrawal | TZS 1,300 | N/A |
| [illegible] | [illegible] | | |
| 1 | CONSUMER LOANS | | |
| | Processing fee | 2% | N/A |
| | Insurance fee | 1.5% | N/A |
| | | | |
| 2 | LOANS | | |
| | Processing fee | negotiable | 2% |
| | Insurance for personal loans | 1.50% | 1.50% |
| | Legal fees | 0.5% minimum of TZS 300,000 | 0.5% minimum of TZS 300,000 |
| 3 | TEMPORARY OVERDAFT (TODs) | | |
| | Processing fee | 2% | 2% |
| SECTION F | TRADE FINANCE | | |
| 1 | Guarantees | | Guarantees |
| | Facility Commission | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qrt. | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qtr. |
| | Arrangement fees | 2% | 2% |
| | Cash Covered | 0.5% per qtr Min 250 per qtr | 0.5% per qtr Min 250 per qtr |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| | Extension to next quarter | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) |
| | Amount increase | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) |
| 2 | Letters of Credit - Imports | | Letters of Credit - Imports |
| | Issuance commision | 0.5% per quarter. Min USD 250. | 0.5% per quarter. Min USD 250. |
| | Handling Fees | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| 3 | Letters of Credit - Exports | | Letters of Credit - Exports |
| | LC Advising Commission | USD 200 flat | USD 200 flat |
| | Amendment advising commision | USD 100 Flat | USD 100 Flat |
| | Correspondences Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Documents handling and examination fee | 0.5% of invoice amount ,min usd 200 | 0.5% of invoice amount ,min usd 200 |
| | Courier charge | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | LC confirmation charges | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) |
| 4 | Letters of Credit Refinancing | | Letters of Credit Refinancing |
| | Interest on refinance | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on refinance | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 5 | Discounting on LC/Invoice/Cheque | | |
| | Interest on discounting | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on discounting | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 6 | Bills Discounting (Bills of exchange including cheques) | | |
| | Interest on discounting | PLR +3%-local; International LIBOR+8% | PLR +3%-local; International Lobor+8% |
| 7 | Documentary Collection - Export | | |
| | Handling charge | 0.25% of the invoice min USD 100 flat | 0.25% of the invoice min USD 100 flat |
| | Courier charge | USD 100 | USD 100 |
| | Corespondence commission | USD 50 Per tracer | USD 50 Per tracer |
| 8 | Documentary Collection - Import | | |
| | Handling Commission | 0.25%. Min USD 100 | 0.25%. Min USD 100 |
| | correspondence Swift charge | USD 50 | USD 50 |
| 9 | Outward Bills for Collection (clean collections & TCs) | | |
| | Handling Commision | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent |
| | Dhl charges | usd 75 flat | usd 75 flat |
| | Returned foreign cheques | claimed charges + locally un re-covered charges | claimed charges + locally un re-covered charges |
| 10 | Inward Bills for Collection | | |
| | Handling Commission | USD 50 flat per collection | USD 50 flat per collection |
| | Swift charged | USD 40 flat per collection | USD 40 flat per collection |
| 11 | Local Currency Transactions | | Local Currency Transactions |
| | Outward remittances (TISS) | TZS10,000 PER TRANSACTION | TZS10,000 PER TRANSACTION |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | NIL | NIL |
| | Inward Swift Transfers (TISS) | NIL | NIL |
| 12 | Foreign Currency Transactions | | Foreign Currency Transactions |
| | Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 |
| | Telegraphic Overseas Charges/ OURS | USD/EUR/GBP 35 -50 MAX FLAT (OURS) | USD/EUR/GBP 35 -50 MAX FLAT (OURS) |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | Inward Swift Transfers | USD 5 FLAT | USD 10 FLAT |
| | International Money Order (IMO) | USD 30 per IMO | USD 30 per IMO |
| | Foreign cheques for collection | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; |
| [illegible] | [illegible] | | |
| 1 | Statements | | Statements |
| | Monthly | FREE | FREE |
| | Adhoc requests | TZS 1,000/ PAGE | TZS 1,000/ PAGE |
| 2 | Cheque Books Issuing | | Cheque Books Issuing |
| | - 25 Leaf | TZS 15,000; USD 10 | N/A |
| | - 50 Leaf | TZS 30,000; USD 20 | N/A |
| | - 100 Leaf | TZS 45,000; USD 30 | TZS 45,000; USD 30 |
| | Counter cheque request | TZS 20,000; USD 10 | TZS 20,000; USD 10 |
| | Cheque Stop payment instructions | leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; | Leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; |
| | Issuance of Manager's cheque | TZS 25,000; USD 20 per item | TZS 25,000; USD 20 per item |
| | Managers cheque cancellation charges | FREE | FREE |
| 3 | Standing order | | Standing order |
| | Standing order set-up | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Standing order maintanance | NIL | NIL |
| | Standing order/Foreign Bank (TT charge) | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 200 | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 200 |
| | Amend / Stop standing Order | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Unpaid standing order | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent |
| 4 | Insufficient funds/effects not cleared | | Insufficient funds/effects not cleared |
| | Insufficient Funds (Refer to drawer) | TZS 50,000; USD 50 | TZS 50,000; USD 50 |
| 5 | Other services/charges | | |
| | Retriving old documents (2-6 months) | TZS 10,000; USD 10 | TZS 10,000; USD 10 |
| | Retriving documents (6 months and above) | TZS 15,000; USD 15 | TZS 5,000; USD 15 |
| | Confirmation/Audit/ Certificate of balance | TZS 30,000; USD 20 or its equivalent | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent |
| | Status enquiry / Reference Letters | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent per customer request | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent |
| | Otward cheque clearing | USD 500 | USD 500 |
| | Salary processing fee | TZS 1,500; USD1 or its equivalent | TZS 1,000; USD1 or its equivalent |
| | Dormant Account Reactivation | FREE | FREE |
| | Cash handling fee-COINS ONLY | 9% of the Deposit | 9% of the Deposit |
| 6 | Soiled notes | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| 7 | Coins | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| | | | |
| | **approved by:** | | |
| | **Signature:** | | **Signature:** |
| | | | |
| | Flavia Kiyanga | | Chomete Hussein |
| | **Chief Operating Officer** | | **Country Chief Finance Officer** |
| | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** | | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** |
| | **Disclaimer: All fees are VAT exclusive.** | | |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mauaji haya yanatia hofu kwenye jamii

**MATUKIO** ya mauaji kutoka ndani ya familia yameendelea kutikisa katika kipindi cha miezi ya hivi karibuni na yanaendelea kutokea na kuleta taharuki kubwa.

Katika vyombo vya habari karibu kila siku kunaripotiwa taarifa za mauaji yakiwamo ya wivu wa mapenzi na mengine ya kutaka kurithi mali kwa nguvu.

Binadamu wamekosa utu na kudiriki kufanya vitendo ambavyo hata wanyama ni vigumu kuvifanya.

Taarifa mbalimbali za watu kuua binadamu wenzao kwa kuwachinja, kujinyonga au kunyonga, kumwagiana petroli na kuchomana moto, havikosi kusikika masikioni na machoni mwa watu.

Katika matukio hayo kunaripotiwa visa mbalimbali vya wanandoa kuuana au kujiua kwa sababu ya wivu wa kimapenzi.

Matukio mengine ni ya watoto kuua wazazi wao kwa tamaa ya kumiliki mali. Ukiangalia visa vyote hivyo vinatokana na watu wa karibu ndani ya familia.

Hali hii inasikitisha na inatisha na kama hatua za haraka hazitachukuliwa familia nyingi zitaendelea kuteketea.

Ni vizuri wataalamu wa mambo ya saikolojia na watu wa ustawi wa jamii wakaingilia kati kudhibiti hali hii isiendelee kuangamiza familia.

Suala hili pia linahitaji nguvu ya pamoja na shirikishi kutoka kwenye familia pale inapoonekana dalili ya kutokea kwa vitendo hivyo.

Kuna baadhi ya wanaodhamiria kufanya vitendo hivyo kwa kumtamkia wazi mtu anayetamka kumdhuru, basi inapotokea hivyo ni vizuri kuripoti mapema kwa ndugu wa karibu au kwa wataalamu wa saikolojia ili liweze kudhibitiwa.

Katika ngazi ya familia wapo wanaoshuhudia dalili hizo mapema pengine kwa watoto kushinikiza wazazi wao kutaka kurithishwa mali mapema badala ya kusubiri mpaka wazazi waage dunia. Kwa kweli hali inatisha na hii yote inasababishwa na tamaa ya kuiga maisha ya watu wengine wenye uwezo na kutaka kufanana nao.

Hao waliofanikiwa walivitafuta kwa kufanyakazi mpaka vikapatikana, hakuna kitu kinachopatikana kirahisi bila kukitolea jasho. Na hili la tamaa ya mali linafanyika sana kwa vijana kwa kuiga maisha ya watu wanaojiposti kwenye mitandao.

Na mara nyingi mauaji hayo yanapofanyika, huyo aliyetekeleza huishia mikononi mwa dola na hiyo mali akiiacha ikiteketea.

Elimu kubwa inahitajika hasa kwa viongozi wa dini kwenye nyumba za ibada kuwasihi watu kumwogopa Mungu.

Mauaji yote yanayofanyika mwisho wake wanaoyatekeleza huishia gerezani au kuharibikiwa kabisa kimaisha.

Kwa wale wanaowaua wenzi wao kwa sababu ya wivu wa mapenzi, ni bora mtu anapoona mwenzake anakwenda kinyume, kukaa kifamilia na kuyazungumza na kama ikishindikana kila mtu atafute njia yake badala ya kutoana uhai. Siku zote hasira ni hasara.

Kila familia ina jukumu la kufuatilia kinachoendelea kwenye familia yao ili kuepusha hali hii inayoendelea kutokea kila kukicha na kuleta taharuki kubwa. Inasababisha hata mzazi kumwogopa mtoto wake aliyemzaa.


Dalili zinapoanza kujitokeza ni vizuri kudhibiti mapema. Moja ya dalili hizo ni mtu kupenda kujitenga peke yake, kutamka maneno ya kuua au kujiua, kuwa mkimya bila sababu, zote hizo zikionekana ziripotiwe na kudhibitiwa.

Ushirikiano ukitolewa vitendo hivyo vya mauaji vitadhibitiwa kwa watu kupewa ushauri nasaha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wazo la kuwapo 'vyumba vya usiri' Mabwepande liwe kitaifa

Na Yasmine Protace

**TAYARI** nchi na zama ilikofika ni haki ya kumtetea mwanamke kuanzia ngazi ya chini aliko, hadi juu katika hatua zingine za umri.

Ni utetezi unaobeba tafsiri pana zaidi, kupitia sura tofauti za madhila ya yanayompata. Huko katika umri wa chini penye hadhi ya usichana, kuna ushuhuda wa mengi sana, maana kuna upungufu wa pili katika umri, mtu hawezi kujimudu vilivyo.

Hiyo ndio moja ya sababu hata shuleni, kunawekewa mkazo huduma muhimu kufikishwa mahali hapo.

Moja ya hatua inayoendelea na kampeni maalum katika sehemu tofauti, ni kuwapo vyumba vya usiri katika shule za msingi na sekondari kusaidia kuwalinda watoto wa kike, dhidi ya namna yoyote ya ukatili dhidi yao.

Inaelezwa, kunapokuwapo vyumba vya usiri kunakozaa tafsiri ya kusaidia kuwatetea watoto wasifanyiwe matendo ya ukatili na hasa wasichana.

Hivi karibuni katika kinachoitwa Bunge la Jamii lililoandaliwa na Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Mabwepande, nje kidogo ya Dar es Salaam, baadhi ya wanajamii waliomba kuwapo vyumba hivyo vya usiri katika shule za msingi na sekondari, lengo ni kulinda mabinti wawe mbali na matukio ya ukatili.

Inafurahisha kumsikia Ofisa Ustawi wa Jamii wa Kata ya Mabwepande, Michael Mihayo, anasema kuwapo vyumba hivyo vya usiri kuwasaidia watoto wakike kusema mambo mabaya wanayofanyiwa na wanaume.

Katika kupambana na matukio hayo ya ukatili ambayo baadhi wananyooshewa vidole mahali hapo, ni vijana wa kiume waendesha bodaboda, sasa kukiombwa shule ziwasaidie mabinti kukabiliana na namna yoyote ya ukatili kwao.

"Kuwapo na vyumba vya usiri sio tatizo, tatizo ni kutokuwa na usiri wa watu," anatamka Mihayo, akisisitiza kuwapo maofisa ustawi wa jamii wa kila shule, wanaopaswa kuwa bega kwa bega kuwasaidia wasichana pale wanapofanyiwa ukatili.

Mtafiti wa Masuala ya Elimu wilayani Kinondoni, Dk. Bille Abrahamu, anasema kuwa changamoto iliyopo katika elimu na uzio katika shule zinatakiwa zitatuliwe kwa wakati na kutokuwapo vyumba vya usiri kunachangia hata msichana mwenyewe inapotokea anafanyiwa ukatili, anakosa pa kuwasilisha malalamiko yake.

Pia anaongeza kila shule itakapokuwa na ofisa wa ustawi wa jamii, ni namna itakayowasaidia kuwapo wanafunzi shuleni kupatiwa faragha ya kuwasilisha siri.

Ni jambo ambalo ukimtathmini Dk. Abrahamu, anasema katika utafiti wake amebaini shule zilizoko katika Kata ya Mabwepande, baadhi zina uzio huku na zingine hazina, akilaumu kutokuwapo uzio katika shule kunachangia tabia ya utoro kutoka kwa wanafunzi.

Pia malalamiko yake yanalenga katika Kata ya Mabwepande anakofanya utafiti kukiwa na maoni kwamba kwa jumla ya shule za msingi nne na sekondari shule moja, ambayo ndio pekee yenye uzio.

Anaongeza kuwa changamoto nyingine wanafunzi wanalazimika kutumia usafiri wa bodaboda na kulipa hadi shilingi 6,000 kwenda na kurudi.

Mtoa hoja huyo, ananena kinachotakiwa sasa ni kufanyike utaratibu wa kuwajengea hosteli mabinti wanafunzi, akiamini zitakuwa mkombozi kwa wasichana hao.

Navutiwa na mtaalamu huyo akisema, serikali ya kijiji inapofanya mikutano ijaribu kuweka utaratibu wa mikutano itakayowasaidia watu kujua kinachoendelea katika kata hiyo.

Mwajuma Juma, katika nafasi yake anaishukuru Asasi ya TGNP Mtandao kwa kuandaa bunge hilo la aina yake, hata kuibua mambo yaliyokuwa yamejificha.

Kuna changamoto nyingine anazozitaja ni uhaba wa maji ambayo hutumika muda mrefu kinadada kwenda kuchota. Pia bodaboda nao inapofika usiku wanapandisha bei maradufu.

Kilio kingine cha Mabwepande, kinaangukia katika kukosekana kituo cha afya kuwahudumia wakazi. Itapendeza yote hayo yakifanyiwa kazi.

# TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA HUDUMA YA KUTOA VIFAA VYA KAZI ZA UWANDANI KWA MRADI WA EACOP.**
**KUMBUKUMBU NA: 0010007360**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika Taasisi zenye Weledi na Uzoefu Kuonesha Nia ya Kutoa Huduma ya Vifaa vya Uwandani (Provision of Field Equipment) kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka eneo la Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Huduma ya Vifaa vya Uwandani Vinavyohitajika ni pamoja na;

- Mahema (Marquee Tents) yenye ukubwa wa saizi ya Kati na Kubwa yenye uwazi wa kufunguka pembeni.
- Viti na Meza za Plastiki na vifaa vya Kutunzia Taka,
- Genereta la Kubebeka kwa Urahisi linatumia petroli lenye ukubwa wa 5KW.
- Nyaya cheneo za umeme zenye urefu wa 5m, 10m na 15m.
- Radio za Mkononi zinazoweza kuchajiwa/Walkie-talkies na vifaa vya kuchajia.
- Sanitiza na Vifaa vya Kunawia Mikono (mobile hand sanitizer).

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi (OSHA).
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.
- Uthibitisho wa uwepo wa vifaa vya kutosha au uwezo wa kuwa na vifaa katika muda mfupi vinapohitajika.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **9:00** mchana Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **21 Januari 2022.** Kichwa cha Barua Pepe ni 0010007360.

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya Makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA HUDUMA YA UHAMISHAJI NA UHIFADHI WA MAKABURI KWA EACOP.**
**KUMBUKUMBU NA: 0010007361**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika Taasisi zenye Weledi na Uzoefu Kuonesha Nia ya Kuandaa na Kutekeleza Mpango wa Uhamishaji na Uhifadhi wa Makaburi yaliyomo ndani ya eneo (Mkuza) lililoguswa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. Mchakato huu utahusisha kuandaa Mikutano na Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa Pamoja Kaya zilizoguswa.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka eneo la Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

Makaburi haya ni yale tu yaliyoguswa na Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki katika Mikoa iliyoguswa na Mradi. Mawanda haya hayajumuishi "Maeneo ya Kipaumbele" au kambi na karakana ya kuandalia mabomba pamoja na eneo la kuhifadhi vifaa lililopo ukanda wa bahari katika Rasi ya Chongoleani.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Huduma za Uhamishaji na Uhifadhi wa Makaburi Utahusisha mambo yafuatayo:

- Kuhakiki maeneo na sehemu makaburi yalipo kama yalivyoainishwa na Mradi.
- Kuandaa Mikutano na Viongozi wa Wilaya na wa Serikali za Mitaa/Vijiji ikiwa ni pamoja na Afisa Afya wa Wilaya ili kuandaa mahitaji yote ya Uhamishaji na Uhifadhi wa Makaburi kwa mujibu wa sheria.
- Kuandaa Mikutano na Kaya zilizoguswa kwa ajili yakuwezesha ufanyikaji wa shughuli za kimila na za kitamaduni pamoja na masuala ya fidia yamelipwa.
- Kuandaa Mikutano na Kaya zilizoguswa pamoja na viongozi wa serikali za Mitaa/Kijiji kwa lengo la kutambua maeneo yakuhamishia makaburi hayo.
- Kushirikiana na Viongozi wa Mitaa/Vijiji kwa ajili ya kutambua vibarua watakaosaidia zoezi la uhamishaji wa makaburi.
- Kuwezesha upatikanaji wa vifaa vyote vya kiafya, kiusalama na kimazingira vitakavyowezesha zoezi la uhamishaji na uhifadhi wa makaburi.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uzoefu wa uhamishaji na uhifadhi wa makaburi nchini Tanzania kwenye maeneo ya viwanda au miradi mingine.
- Uzoefu wa kushirikiana na mamlaka husika kwenye shughuli za uhamishaji na uhifadhi wa makaburi Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi (OSHA).
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **9:00** mchana Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **21 Januari 2022.** Kichwa cha Barua Pepe ni 0010007361.

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya Makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

# RC Makalla azidisha mbinu uandikishaji watoto shule

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewataka wazazi na walezi kuwapatia watoto wao haki ya kupata elimu akisisitiza kuwaandikisha kwa wakati wale wote wenye uhitaji wa darasa la awali, la kwanza na kidato cha kwanza.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, alisema siku tano zilizopita uandikishaji wa watoto kwa shule za awali ulikuwa asilimia 32 na msingi asilimia 52, huku akibainisha kuwa katika uandikishaji huo ni Ilala tu ambayo iliandikisha zaidi ya asilimia 50.

Makalla alisema baada ya jitihada za makusudi kufanyika, usajili umeongezeka hadi asilimia 68.9 kwa shule za msingi.

Aliwataka wazazi kuongeza kasi ya kuwaandikisha watoto ili kufikia malengo, huku akiwataka wakuu wa shule kuondoa vikwazo vinavyowafanya wazazi waone ugumu katika kuwaandikisha watoto.

"Katika hizi siku zilizobaki watoto wote waruhusiwe kwenda shuleni na wazazi wawajibike watimize majukumu yao ya kuwapa watoto elimu. Kama una mtoto anastahili kwenda awali basi aende, kama anastahili kwenda shule ya msingi aende na kama ni sekondari pia aende. Hakuna urithi mkubwa duniani kama kumpa mtoto wako elimu," alisema Makalla.

Pia aliwataka wakuu wa wilaya na wakurugezi kuitisha mikutano kila mtaa kuzungumza na wazazi ili kufikisha ujumbe wa kuwaandikisha watoto shuleni, akitaka kufanyika kwa sensa ili kujua idadi ya watoto walioenda shule na wasioenda.

Aidha, aliwataka wakurugenzi kutumia fedha za ndani kuimarisha miundombinu ya shule ikiwamo kuongeza matundu ya vyoo yanayoendana na idadi ya wanafunzi huku akishauri shule mpya zilizoko katika mkakati wa kujengwa, zijengwe kwa mfumo wa ghorofa kutokana na uhaba wa ardhi.

Makalla aliagiza kuwa ndani ya siku 21 watendaji wa mitaa na kata wawasilishe kwa wakurugenzi taarifa ya shule zote katika maeneo yao zenye migogoro ya ardhi inayotokana na watu kuvamia ardhi za shule, akidai kuwa amejipanga kutatua changamoto hizo.

"Mkoa wetu uko katika kampeni mbalimbali, ikiwamo ya Safisha Pendezesha Dar es Salaam. Kwa hiyo shule haiwezi kuwa kisiwa, hivyo naomba mshiriki vizuri, maeneo yenu mandhari ya shule myatunze. Tutawaletea vifaa vya kuhifadhia uchafu kila tunavyopata," alisema Makalla.



Madereva wa bodaboda wakipita kwenye barabara ya mabasi ya mwendokasi katika Barabara ya Morogoro, Kimara Baruti, mkoani Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni uvunjifu wa sheria ya usalama barabarani. PICHA: SABATO KASIKA

# Bil. 5.6/- kuboresha barabara

**Na Samson Chacha,** TARIME

HALMASHAURI za Mji Tarime na Wilaya ya Tarime, zimepanga kutumia Sh. 5,615,604,643.37 katika bajeti ya barabara kwa mwaka wa fedha wa 2022/23 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 564.98.

Kiasi hicho cha fedha pia kitatumikwa kwa ajili ya ujenzi wa madaraja saba, makalavati 299. Kwa upande wa barabara zitakazojengwa ni kilometa 3.93 kiwango cha lami, kilometa 370.96 changarawe, udongo kilometa 190.09, mlisho kilometa 226.11 na barabara ya jamii kilometa 194 .97.

Sambamba na barabara na madaraja hayo, sehemu ya fedha hizo inatarajia kutumika kuweka vigingi vya kulinda eneo la hifadhi ya barabara na kujenga mitaro ikiwamo ya kutolea maji ya mvua.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Tarime, Charles Marwa, alisema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha barabara zote zinakuwa na viwango na kupitika mwaka mzima.

Marwa alisema katika fedha hizo, Sh. 712,954,500 zitatumika katika kufungua barabara yenye urefu wa kilometa 5.6 kutoka Kijiji cha Mogabiri kwenda Nyarwana.

"Jumla ya mikataba mitano yenye thamani ya Sh. 1,002,477,976 ilitiwa saini hadi kufikia Desemba, mwaka jana na kilometa 116.39 zilifanyiwa matengenezo pamoja na ujenzi wa makalavati 10.

"Changamoto zinazoikabili TARURA ni pamoja na jamiikutolewa umuhimu wa kulinda na kutunza barabara, kwa kupitisha mifugo katikati ya barabara pamoja na malori makubwa zaidi ya tani 10 kuharibubarabara za udongo wakati wa mvua," alisema.

Kutokana na hayo, alisema TARURA itatoa elimu kwa wananchi na viongozi wa vijiji na kata kuwaelimisha kutii sheria ili kutoharibu alama na mabango yaliyowekwa kandokando ya barabara na kutunza barabara kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Pia alisema TARURA itaanza kuchukua hatua kukamata malori na wananchi wanaoharibu barabara.

# Shirika laomba wafadhili kusaidia watoto mapacha

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali linalojishughulisha na huduma kwa familia zenye watoto mapacha zisizo na uwezo, Eden Twins Foundation, linatafuta ufadhili ili kupanua shughuli zake nchi nzima. Mwenyekiti wa Shirika hilo, Diana Joy Mbena, alisema kwa sasa maskani yake yako Kibaha mkoani Pwani na mikakati yao ni kupanua kazi za shirika hilo.

Alisema, kutokana na uchanga na ukosefu wa ufadhili wa kifedha ambao ungesaidia kufikia mikoa mingi zaidi, wameanzia mkoani Pwani.

"Baada ya uzinduzi wa tamasha la kutambua mapacha uliofanyika jijini Dar es Salaam mwaka jana, nimekuwa nikipokea simu za familia zenye mapacha kutoka maeneo mbalimbali nchini zikihitaji msaada," alisema Diana.

Alisema kwa sasa anaendelea na mchakato wa kusaka fedha kwa wafadhili ambao anaamini wakimwezesha, anaweza kuzunguka katika mikoa mbalimbali kutambua familia zenye mapacha zisizo na uwezo wa kiuchumi na kutafuta njia ya kuzisaidia.

"Kwa simu ambazo nimekuwa nikipokea, ni wazi kwamba kuna familia nyingi zenye watoto mapacha zisizo na uwezo kiuchumi, hivyo ni vyema jamii, wadau mbalimbali tukashirikiana kuzisaidia familia hizo," alisema.

Alisema, wadau na baadhi ya wafadhili wamekuwa wakisaidia makundi mbalimbali yakiwamo ya watu wenye ulemavu, wasiojiweza na kwamba familia zenye mapacha zisizo na uwezo ni kama zimesahaulika.

"Ninadhani ni wakati sasa jamii kuangalia uwezekano wa kutambua familia za aina hiyo na kusaidiana nasi Eden Twins Foundation kuzisaidia kwa hali na mali kuliko kuziacha zikihangaika," alisema.

Alisema, familia nyingine zinakuwa na mapacha hadi 10 na hazina uwezo wa kuwahudumia hali inayosababisha watoto wakose hata vifaa vya shule, kama madaftari, sare na vitu vingine muhimu.

"Ukikutana na familia ya aina hiyo, basi ujue kuwa hata uwezo wa kupata mlo mmoja nao ni shida, hivyo ninaomba tushirikiane kuzisaidia kwa hali na mali, kwani hata mimi shirika langu bado ni changa," alisema.

Kadhalika, alisema familia zenye mapacha zikitambuliwa kama ilivyo kwa makundi mengine yenye uhitaji, zinaweza kusaidiwa na kupunguza ugumu wa maisha unaozikabili.

## Mamia wajitokeza kuchunguzwa afya jopo madaktari wa Pakistan

**Na Salome Mwasamale**

MKE wa Rais mstaafu wa Awamu ya Tano Zanzibar, Salma Salmin Amour, ameongoza mamia ya wananchi waliojitokeza kupima afya zao kwa hiari huduma inayoendeshwa na jopo la madaktari bingwa wa Jeshi la Wanamaji kutoka nchini Pakistan.

Akizungumza na Nipashe baada ya kupata huduma hiyo, Salma aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kupata huduma ya vipimo na matibabu bure.

Aliwashauri Watanzania kutumia fursa hiyo ya kupata matibabu na dawa walizokuja nazo mabingwa hao ili wasirudi nazo nchini kwao.

"Nawashauri Watanzania wajitokeze kwa wingi kupata huduma hii ya upimaji na matibabu ili hizi dawa nyingi na nzuri walizokuja nazo wasirudi nazo kwao," alisema.

Naye balozi wa Pakistan nchini Tanzania, Muhammad Saleem, alisema huduma hiyo ya siku mbili linalenga kuhudumia watu 3,000 na mpaka juzi watu 600 walijitokeza kupata huduma hiyo.

Kutokana na mwamko huo kuwa mdogo, aliwashauri wananchi kujitokeza kwa wingi kupata huduma hiyo ili kuendelea kudumisha uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na Pakistan.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, aliwataka wananchi kuitumia vizuri fursa hiyo adhimu kutoka Pakistan ambayo imekidhi vigezo vya huduma za afya.

"Naomba Watanzania popote walipo wajitokeze kupima afya zao kwa kuwa madaktari waliopo ni wazuri na wamebobea katika masuala ya huduma ya afya ya jamii," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wapakistan waishio Tanzania, ambao ndiyo wenyeji wa ugeni huo, Muhammad Mushtaq, alisema ugeni huo umekuja kutokana na uhusiano mzuri uliopo kati ya nchi hizo mbili.

Alisema hii ni mara ya pili kwa jopo hilo la madaktari kutoka nchini Pakistan kutoa huduma kama hiyo nchini na kabla ya kuja Tanzania walikuwa nchini Ghana.

Baadhi ya huduma ya upimaji inayotolewa ni pamoja na ganzi, shinikizo la damu, kinywa na meno, sukari, mifupa, malaria, UTI na macho.

# Walioahidiwa mashamba ya korosho Manyoni wamshtakia RC

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Manyoni mkoani hapa, inadaiwa kupokea zaidi ya Sh. milioni 600 za wananchi waliowaahidi kuwapatia mashamba ya kulima korosho bila kuwapatia mashamba hayo kwa miaka minne sasa.

Kutokana na malalamiko ya wananchi waliotoa fedha hizo kwa kuziweka kwenye akaunti maalumu ya halmashauri kama walivyokuwa wameelekezwa, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, aliitisha kikao cha kamati tendaji ya mradi wa korosho Manyoni na Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa, aligiza kufungwa akaunti zote za kupokea fedha za ununuzi wa mashamba hayo hadi utakapofanyika uhakiki wa kujiridhisha.

Naye Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Mahenge, aliiagiza kamati hiyo hadi kufika Jumatatu Januari 17, mwaka huu, iwe imetoa taarifa ya mradi huo iliyo sahihi ambayo itapitiwa na Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) kabla ya kuwasilishwa kwa Mkuu wa Mkoa.

Dk. Mahenge aliagiza kuandaliwa upya kutokana na taarifa iliyokuwa ikitolewa kutojitosheleza baada ya majina ya baadhi ya watu wanaodaiwa kulipia fedha kutokuwapo licha ya kuwa nayo na kiasi cha fedha kilichopokelewa kikiwa hakijabainishwa.

"Taarifa hiyo muiandae vizuri najua hizo namba mnazo nendeni mkaziunganishe na muwe makini kama kuna watu walikuwa wakiingiza fedha hizo benki mnapaswa kuwajua, wapo walioleta fedha hizo ofisini, mliowapa mashamba, ambao bado hamjawapa, waliopanda au kupalilia hivyo nawaombeni tengenezeni taarifa inayojitosheleza," alisema Dk. Mahenge.

Alisema haiwezekani wapokee fedha za mtu halafu wakashindwa kuandaa taarifa kwa kuwa jambo hilo sio geni kwao na kama taarifa hiyo inashindwa kuandaliwa vizuri patakuwa na kizungumkuti, taarifa hizo huenda zitakuwa kwa mtu mmoja bila kushirikishwa wengine na hawajui, lakini kama wajumbe wote wa kamati hiyo wangekuwa wanajua isingeshindwa kuandaliwa.

"Mkurugenzi, Mkuu wa Wilaya nawaombeni taarifa hii ikaandaliwe upya ili tupate uwazi taarifa ionyeshe toka mlipoanzisha mradi huu mlitenga eneo kiasi gani, watu wangapi walioleta maombi na kulipa, masharti yenu yalikuwaje, gharama za usafiri ilikuwa ni shilingi ngapi, gharama za fomu, michango iliyotolewa kama zahanati na mingine ilikuwa kiasi gani na barabara vitu vyote viainishwe na ioneshe fedha mlizopokea kama zipo sawa na zile zilizoko benki na kama zipo ambazo mlizipokea na hamkuzipeleka benki pia mzionyeshe," alisema Dk. Mahenge.

Alisema anataka tatizo hilo walimalize na kuwa jambo hilo anamwachia mkurugenzi na lifanyike chini ya Katibu Tawala na sio kuiachia kamati peke yao.

Alisema kama watashindwa kupata mzani waende kwenye mashamba kujiridhisha kwa kuhakiki majina ya wamiliki wa mashamba hayo.

Alisema taarifa hiyo pia ionyeshe fedha zilizopokelewa kama mashamba yake yapo kwa kuwa kuna uwezekano wa fedha zilizoingizwa kuwa ni zaidi ya ekari za mashamba walizonazo na waeleze kuwa kutokana na kutofunga akaunti walipokea fedha hizo ili kama kutakuwa na uwezekano watu hao ambao watakosa maeneo watafutiwe sehemu nyingi kama Itigi au Ikungi kwa makubaliano kwa sababu shida yao ni kupata mashamba.

Naye Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri ya Manyoni ambaye ni mjumbe wa kamati hiyo, Lweikiza, alisema taarifa kamili ya mchakato wa mradi huo tangu kuanza na matumizi yote ya fedha ipo na wataiwasilisha kwa Mkuu wa Mkoa.



Tangi la maji lililowekwa kwenye kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam, kwa ajili ya abiria kunawa mikono ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, likiwa limetelekezwa na mamlaka husika kwa muda mrefu sasa bila ya kuwekwa maji. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TARURA yatenga Sh. bilioni 1 matengenezo barabara korofi

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), mkoani Mtwara imesema kuwa imetenga Shilingi bilioni tano kwa ajili ya matengenezo ya barabara korofi za ndani ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Mtwara, Mhandisi Hatibu Nunu, alitoa taarifa hiyo alipokuwa akiwasilisha mpango wa bajeti ya matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, katika kikao maalumu kilichofanyika mjini hapa.

Alisema katika fedha hizo Sh. 1,795,300,000 zitatolewa na Mfuko wa Barabara (Road Fund) kwa ajili ya kutengeneza barabara zenye urefu wa kilomita 234.71 na kilomita 215.72 ni za matengenezo ya kawaida.

Mhandisi Nunu alisema Sh. 411,020,000 zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na pia Sh. 505,140,000 zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi zenye urefu wa kilomita 17.5.

Alisema Sh. 582,000,000 zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya muda maalumu na zitakuwa kilomita 1.94.

Mhandisi Nunu alisema matengenezo mengine ni pamoja na ujenzi wa makalavati sita na fedha iliyotengwa ni Sh. 160,940,000 kwa ajili ya shughuli hiyo.

Alisema Sh. 96,160,000 zimetengwa kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji na Sh. 31,040,000 kwa ajili ya utawala. Nunu alisema barabara zingine zenye urefu wa kilomita 3.4 zitatengenezwa kwa kiwango cha lami kupitia fedha za maendeleo za mfuko wa barabara ambazo ni Sh. 2,236,000,000.

Alisema kilomita mbili zitatengenezwa kupitia fedha za tozo na nyongeza ya bajeti jumla ya Sh. 1,000,000,000 na kueleza kuwa hadi sasa Manispaa ya Mtwara-Mikindani ina barabara zinazosimamiwa na TARURA zenye urefu wa kilomita 384.79. Mhandisi Nunu aliongeza kuwa katika kilomita hizo za zilizotengenezwa kwa kiwango cha lami ni 50.61 za changarawe 72.54 na za udongo ni kilomita 261.64.

Vile vile, alisema manispaa ina vivuko 632 yakiwamo makalavati 630 pamoja na daraja moja na drift moja lengo ni kuhakikisha mji wa Mtwara unakuwa na mwonekano wa kuvutia katika miundombinu yake.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, aliiagiza TARURA inapopanga mipango yao hasa bajeti kukutana na ngazi zingine ikiwamo Baraza la Madiwani ili mpango huo upewe baraka na madiwani kupitia kikao chao kama ilivyofanyika hivi sasa.

Naye Mbunge wa Jimbo la Mtwara, Hassan Mtenga, aliwasihi madiwani kuacha kuilalamikia TARURA katika matengenezo ya barabara kwa sababu taasisi hiyo pia inachangamoto zake ambazo kwa namna moja au nyingine wakati fulani zinakwamisha utendaji kazi wao.

# Mjema ashauri uhudhuriaji kliniki kwa uzazi salama

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amewataka wajawazito mkoani humo, kujenga tabia ya kuhudhuria kliniki mara kwa mara ili kupewa elimu ya afya ya uzazi na kujifungua salama.

Mjema alibainisha hayo juzi wilayani Kishapu alipokuwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maendeleo na kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa Zahanati ya Negezi iliyoko Ukenyenge wilayani humo, ina kataa kuzalisha wajawazito wa uzao wa kwanza na wa tano.

Alisema ni kweli zahanati huwa hazizalishi wajawazito wa uzao wa kwanza na kuwataka wawe wanahudhuria kliniki mara kwa mara ili kupewa elimu ya afya ya uzazi, pamoja na kujua maendeleo ya mtoto ili siku ya kujifungua wawahi hospitali na kuzaa salama.

"Mjamzito anapohudhuria kliniki hawezi kupata shida wakati wa kujifungua, shida yenu huku vijijini huwa hamuendi kliniki, mkishikwa uchungu ndipo mnakimbilia kwenye zahanati jambo ambalo ni hatari," alisema Mjema.

"Lakini mkihudhuria kliniki mtapewa elimu ya afya ya uzazi pamoja na kujua maendeleo ya mtoto na wale wenye uzao wa kwanza na wa tano mtaambiwa mkajifungue kwenye hospitali kubwa, sehemu ambayo ni salama kwenu kuliko kwenye zahanati," aliongeza.

Aidha, aliwataka wahudumu wa afya ngazi ya jamii kuendelea kutoa elimu kwa wajawazito, wahudhurie kliniki mara kwa mara na kuwataka pia wauguzi ngazi ya zahanati kuwa mjamzito akifika usiku anaumwa uchungu licha ya kuwa na uzao wa kwanza, wamzalishe ili asije akapoteza maisha na mtoto.

Katika hatua nyingine alisema, kutokana na Kata ya Ukenyenge kuwa na idadi ya watu wengi, tayari serikali imeshaanza kuipanua zahanati ya Negezi ili kuigeuza kuwa kituo cha afya na ujenzi wake upo hatua ya upauaji kwa gharama ya Sh. milioni 250.

Awali, wananchi wa Negezi walitoa malalamiko kwa Mkuu huyo wa Mkoa kuwa wauguzi wa Zahanati ya Negezi, wanakataa kuzalisha wajawazito wa uzao wa kwanza na wa tano na kupata shida ya kwenda kupata huduma umbali mrefu katika Hospitali ya Wilaya Kishapu au ya rufani mkoani Shinyanga.



Mkazi wa Dar es Salaam, Abigael Emmanuel akimjaribisha shati mtoto wake, Helena Athuman Mdoe, wakati akifanya manunuzi ya vifaa vya shule katika Soko la Karume jijini humo mapema wiki hii, kwa ajili ya maandalizi ya kuanza darasa la kwanza Januari 17, mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watoto wenye mahitaji maalumu kujengewa bweni

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

JUMUIYA ya wanafunzi na walimu wa shule ya msingi Tunduru mchanganyiko wilayani hapo, wameipongeza serikali kwa kuwapatia Sh. milioni 80 kwa ajili ya kujenga bweni litakalotumika kwa watoto wenye mahitaji maalumu wanaosoma shuleni hapo.

Shukrani hizo zimetolewa na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Twalib Jafari.

Mwalimu Jafari alisema bwalo hilo ni ukombozi kwa watoto hao kwa kuwa baada ya kukamilika watoto wote wenye mahitaji maalumu wakiwamo wanaotoka maeneo ya mbali kulala hapo.

Mwalimu wa kitengo hicho, Maths Ndunfuru, alisema kwa sasa shuleni hapo kuna watoto 39 wakiwamo wasichana 11 na wavulana 28.

Akizungumzia ujenzi wa bwalo hilo, Ndunfuru alisema utasaidia kuongeza idadi ya watoto zaidi kwenda kusoma shuleni hapo.

Akiongea kwa niaba ya wananchi, Diwani wa Kata ya Mlingoti Mashariki, Namka Luambani, alisema wamepokea mradi huo kwa furaha na wamejipanga kukamilisha kwa wakati ili kutoa nafasi kwa watoto hao kuanza kupata huduma kwa wakati.

Alisema mradi huo ni muhimu kutokana na shule hiyo kuwa na uhitaji na kwamba kikamilika kwake itakuwa ni kivutio kwa wazazi wenye watoto wa aina hiyo kupeleka watoto wao kusoma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Chiza Marando, alisema fedha hizo zimetolewa na serikali kwa ajili ya kutatua changamoto ya muda mrefu iliyokuwa ikiikabili shule hiyo ambayo watoto wenye ulemavu wa kutosema (bubu) viziwi, mtindio wa ubongo na ulemavu mwingine, kwenda shuleni na kurudi majumbani kwao hali iliyoonekana kuwa kikwazo kwa wazazi na walezi wengi kuwaruhusu kwenda kusoma.

Kutokana na hali hiyo Marando alitoa wito kwa wazazi na walezi wenye watoto wenye ulemavu kuwapeleka shuleni hapo kwa kuwa mazingira yameboreshwa watoto wao watasoma na kuishi hapo katika kipindi chote cha masomo yao.

# Wakazi Mbezi waondolewa hofu watoto wao kujiunga shule sekondari

**Na Salome Mwasamale**

WANANCHI wa Kata ya Mbezi, Manispaa ya Ubungo wenye watoto waliofaulu kidato cha kwanza na kupangwa katika Shule ya Sekondari mpya ya Mbezi Makabe, wametakiwa kuwa watulivu katika kipindi hiki serikali inachoandaa utaratibu watakavyojiunga na kuanza masomo yao shuleni hapo.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Diwani wa Kata ya Mbezi, Ismail Malata, aliwataka wananchi wa Mbezi kuondoa hofu kwa kuwa serikali inaendelea na mchakato wa kukamilisha taratibu zote zinazohitajika ukiwamo ule wa aina ya sare wanazotakiwa kuvaa watoto hao.

"Nawaomba wazazi na walezi wawe watulivu serikali bado inaendelea na mchakato wa kuikamilisha shule hiyo mpya iliyofunguliwa hivi karibuni na watatangaziwa namna ya kuwaleta watoto wao na kuanza masomo kama ilivyo kwa shule nyingine," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Makabe, Peter Tambwe, alisema vikao vya kuimarisha mikakati ya uanzishwaji wa shule hiyo vinaendelea ili kuhakikisha watoto wanajiunga na kuanza masomo Januari 17 kama ilivyopangwa na serikali.

Tambwe alisema ujenzi wa sekondari hiyo ni moja ya kipaumbele ambacho kimeondoa changamoto iliyokuwa ikiwakabili watoto wa Kata ya Mbezi na ni lazima ianze kazi kama ilivyopangwa.

Alisema Shule ya Msingi Makabe hubeba zaidi ya wanafunzi 2,500 kila mwaka ambao walikuwa wakifaulu na kupangwa katika shule za kata jirani ambako ni mbali na eneo wanalotoka na kuona ni bora wapambane ili ipatikane sekondari ya Mbezi Makabe ambayo tayari imekamilika.

"Shule mpya ya Sekondari Mbezi Makabe imekamilika kwa kila kitu ikiwamo majengo, vyoo, madawati na ofisi za walimu hivyo hakuna sababu itakayosababisha watoto wasiripoti shule Januari 17, nawaomba wazazi wawe watulivu wakati mipango inaendelea," alisema.

Awali, wakizungumza na Nipashe baadhi ya wazazi ambao watoto wao wamefaulu na kupangwa shuleni hapo, walionyesha wasiwasi wa watoto wao kuripoti shuleni hapo kwa kuwa mpaka sasa hakuna maandalizi wanayoona yanafanyika kwa watoto wao.

ama
ALHAMISI JANUARI 13, 2022
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

TV inavyohatarisha usalama afya, makuzi, saikolojia ya ukuaji mtoto



Ukurasa 13

Wataalamu: Chanjo inakukwepesha Corona, ikikupata hutalazwa wodini



Ukurasa 14

**MTAFITI DK. AHMED ALI:**
**Dhahabu, manukato na ubani tiba mpya ya saratani, pumu**

# Walimu wanapobeba lawama kuu za kisaikolojia, afya kwa wanafunzi

**Na Sophia Mwilawa, SJMC**

SHERIA, pia Sera ya Elimu nchini inaelekeza elimu ya msingi kitaifa ni ya lazima kwa watoto wote. Pia, Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, inaelekeza mwaka wa kimasomo unatimia kwa mtoto kuwa shuleni siku 194, kati ya 365 za mwaka.

Maana yake asilimia 53 (zaidi ya nusu ya muda) wa mtoto wa elimu ya msingi anakuwa shuleni ikizingatiwa umri wao wote unaangukia utoto.

Sera ya Elimu ya Msingi inataja siku tano za kila wiki, mtoto anapaswa kuwa shuleni kila siku ikimchukua si chini ya saa nane hadi 10 akiwa katika mazingira ya shule, kati yake zaidi ya saa sita ni lazima kuwa darasani.

Kimsingi, Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inamtambua mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka 18 na wakati wote anasimamiwa rasmi na ama mzazi au mlezi.

Kwa tafsiri pana, wanaowajibika na malezi ya mtoto moja kwa moja kwa muda mrefu ni shule, mzazi na mlezi na wawapo shule, wanaohusika kulea, pia kuwafunza ndani na nje ya darasa ni walimu, wakisaidiana na watumishi wengine, hata wanabaki kuwa miongoni mwa watu muhimu katika malezi ya watoto.

Kwa mwanafunzi bwenini, tafsiri pana ya ulezi inawaangukia walimu na watendaji shuleni, wanaodumu nao kwa saa 24, zikiwamo siku za mapumziko mwishoni mwa wiki.



Mwalimu akiwa kazini darasani na wanafunzi wake. **PICHA: MTANDAO**

### PENYE UTATA

Baadhi ya walimu licha ya taaluma yao kuwakasimu ulezi, inadaiwa wanashiriki kukatishwa ndoto za watoto kisaikolojia na kiafya, kutokana na mienendo yao isiyoridhisha.

Sheria ya Watoto, 2009; Sura 9(3)(c) inatamka muda wote wa masomo wa mwalimu anakasimiwa jukumu la kulea kupitia kifungu cha sheria kinachotamka:"Kwa muda ambao mzazi hatakuwapo, mtoto atapata malezi toka kwa mtu anayefaa (kama walimu)..."

### TUME YA WALIMU

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Profesa Willy Komba, katika ripoti yake kuhusu maadili ya kazi ya ualimu, anasema mwaka 2020/2 kuna makosa makubwa yamejitokeza kwa walimu zikiwamo za utoro, kughushi vyeti, uhusiano kimapenzi, ukaidi na ulevi.

Kunatajwa makosa 1,795 yaliyoripotiwa yanayowahusu walimu 184, kati ya Julai 2020 hadi Septemba 2021, kinara wao ni utoro na walimu 931 sawa na nusu (asilimia 51.9) ya makosa yote. Pia, kuna mikasa ya mapenzi 211, ikiwa asilimia 11.8 ya makosa yote.

Profesa Komba anafafanua elimu kwa ujumla imejikita katika maadili, hivyo panapokosekana maadili hakuna elimu, hivyo 'kuelimika'.

"Tunachoona kinachoendelea madarasani, walimu wetu na walimu wenye vipindi vya dini. Hii sio sawa, kwani kazi ya ualimu ikiweka maadili pembeni inakuwa haijakamilika," anasema Profesa Komba.

### MWANASAIKOLOJIA

Mwanasaikolojia kutoka Hospitali ya Manispaa ya Ubungo Dk. Hashim Limila anafafanua: "Mtoto ana uwezo wa kuiga vitu kwa haraka bila ya kujali ni kizuri au kibaya na athari zake huonekana baada ya muda mfupi au mrefu hususani wanafunzi wa shule za msingi ambao wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya ajabu.

"Athari hizo ni pamoja na msongo wa mawazo, kwani mwanafunzi huwa njia panda, haelewi ni njia gani sahihi kwake, kukosa kujiamini hususani anapokuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwalimu, kutofanya vizuri darasani kwa kukosa elimu bora kwani walimu wanafundisha wakiwa wamelewa, kutengwa na jamii kutokana na tabia zisizofaa, kubadilika na kuachana na malezi ya wazazi wake na kuharibikiwa kimaisha kabisa.

"Tunawaamini walimu na ndio maana tunawapeleka watoto wakapate elimu sio tu ya darasani, pia ya maisha kwa ujumla, mavazi ya walimu hususani wanawake yamekuwa ni mafupi..."

### UTETEZI WA WALIMU

Baadhi ya walimu wanajitetea sababu kubwa ya mmomonyoko wa maadili ni utandawazi unaowaingiza kuiga yasiyofaa, hususani walio vijana.

Pili Samwel (sio jina lake halisi), ni Mwalimu wa Shule ya Msingi Makole, Dodoma anaeleza: "ili kupunguza mmomonyoko wa maadili kwa walimu, ni vyema kuwapa utaratibu wa kukumbushana maadili ya taaluma, kwa kufanya semina za mara kwa mara.

INAENDELEA UK.12

AFYA

# TV inavyohatarisha usalama afya, makuzi, saikolojia ya ukuaji mtoto

**Na Maira Levi Blyden,** SJMC

KUNA uhusiano wa karibu baina ya afya, mazingira na msaada wao ni habari. Vyote vinategemeana, hali kadhalika ndio inabeba picha ya nafasi ya madhara.

Wataalamu wanasema mimba inapotungwa, huashiria mwanzo wa hatua za awali katika malezi na makuzi bora kwa mtoto, huku msemo wa Kiswahili unaodaka mantiki hiyo ya kiafya, saikolijia na elimu kwamba "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo."

Mbali na mahitaji ya moja kwa moja kiafya, pia mazingira anakopatikana mhusika ni muhimu ama kumdhuru au kumlinda.

Utafiti unaonyesha elimu duni ya wazazi na walezi kuhusu malezi na makuzi ya mtoto inachangia sana katika udumavu wa watoto kimwili, kiakili na kisaikolojia.

Maudhui yanayozalishwa na vyombo vya habari hususan televisheni zikiwamo filamu, maigizo, muziki na habari yanatajwa kuwa na mchango mkubwa sana katika malezi na makuzi ya mtoto iwe katika namna chanya au hasi.

Hata hivyo, katika saikolojia na maudhui ya Kongamano la Umoja wa Mataifa la Haki za Mtoto (UNHRC) yanasema: "Kila mtoto ana haki ya kupata habari mbalimbali za kitamaduni, kitaifa na kimataifa kutoka kwa vyombo vya habari.

"Hivyo basi, vyombo vya habari vinapaswa kutoa habari ambazo watoto wanaweza kuelewa na zisiwadhuru," inafafanua.

Kanuni na sheria za mawasilano zilizoko, zinaelekeza namna mtu anapoenda kwenye Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasliano Tanzania (TCRA) kuchukua leseni ya urushaji matangazo, kuna miongozo wanayotoa kuhusu maudhui yanayopaswa kurushwa na yale ya kudhibitiwa.

"Ila sisi kama Mlimani (TV na Radio) kwa kutambua hilo, tumekuwa tukizingatia maagizo hayo ili kuwalinda watoto na maudhui yanayowazidi umri.

"Tunavyo vipindi vya watoto," anatamka Amos Gomba, Mhariri katika vituo vya Mlimani Radio na Mlimani TV, vinavyomilikiwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).



Watoto waliokusanyika kuangalia televisheni nyumbani. **PICHA: MTANDAO**

> **Wakati wazazi wengine wakiwapatia uhuru watoto wao kutazama chochote kinachoonekana kwenye runinga, hali isiyoonekana kwa wengine.**

### KUTOKA KWA WAZAZI

Suala la malezi linabainika kuwa mtambuka na haliishii katika chakula, mavazi na malazi. Uwajibikaji unafikia wazazi na walezi kusimamia miongozo ya utazamaji maudhui ya vyombo vya habari, hususani televisheni.

Baadhi ya wazazi wameeleza namna wanavyowasimamia watoto wao, akiwamo anayejitambulisha kwa jina, Mama Joyce mkazi wa Kijitonyama, Dar es Salaam.

Mzazi huyo ana maoni: "Niliwahi kumshuhudia mwanangu anatazama filamu ya mapigano, nikamuuliza, anataka kuwa bondia? Nikamwambia anapaswa kutizama vitu vya kumfundisha. Nilichofanya nikazima runinga japo alikasirika."

"Mimi mwanangu hawezi kutazama runinga bila ruhusa yangu na nisipokuwepo nyumbani, ni lazima amuombe mama yake ndio aruhusiwe na pale kwangu hakuna 'CD' za kidunia," anatamka mzazi anayejitambulisha kwa jina Baba Kyamarisi.

Baadhi ya Wazazi wanasema uwajibikaji wao katika suala zima la malezi na makuzi ya watoto linachangamoto zake na katika maoni yao wanasisitiza ni wakati mgumu kumkataza mtoto asitazame runinga, itakuwa ngumu kwa sababu wana simu na vitu vingi vya mawasiliano.

Changamoto kuu inayotajwa ni hata mtoto akidhibitiwa nyumbani, akiwa kwingine anafikiwa na mawasiliano hayo, kwa maana inategemea kiwango cha udhibiti mahali aliko.

Msingi wa maudhui ya vyombo vya habari, ina zalishwa kulingana na aina ya watazamaji, umri na hata muda unaofaa kuyarusha.

Kanuni Mpya ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta EPOCA ya Mwaka 2018, inatoa mwongozo na kanuni za maudhui ya utangazaji wa redio na televisheni katika kuwalinda watoto dhidi ya maudhui yasiyofaa, yakiwamo ya ngono, ubaguzi wa rangi, mauaji, unyanyasaji, mapigano na yanayofanana nayo.

Aisha Mbuma, mkazi wa Dar es Salaam, anatamka: "Wazazi kwa kutokujua wamekuwa wakitazama vipindi vinavyowazidi umri watoto wakiwa na watoto bila hata ya kushituka, mazoea ya kuchukulia vipindi vyote ni sawa, limekuwa likiwaingiza wazazi mtegoni".

Ni wazi watoto wanapenda kutazama na kusikiliza maudhui mbalimbali ya vyombo vya habari hususan ya televisheni, hivyo usimamizi unahitajika, hali ambayo baadhi ya watoto waliozungumza na mwandishi wa makala hii, wanakiri ni watazamaji wa televisheni kwa muda mrefu.

### MTAALAMU SAIKOLOJIA

Mwanasaikolojia Ester Magita, anasisitiza jamii kuwa na kawaida ya kutoa miongozo ya televisheni kwa watoto wao na wazazi waache kuwa tegemezi wa upande wa malezi ya mtoto, kwa kuiachia runinga kazi ya malezi, badala yake wazisimamie nafasi zao kikamilifu.

"Mtindo wa malezi uliopo kwenye familia unaharibu maadili yetu. Leo hii mtoto akilia kidogo tu anabembelezwa na katuni, wakati fulani ili mtoto ale anaahidiwa kutizama katuni, jambo ambalo si jema kwa akili ya mtoto mwanzo inamfanya adumae kwa kuona suluhu ya kila jambo kwake ni katuni".

Anasema, wakati wazazi wengine wakiwapatia uhuru watoto wao kutazama chochote kinachoonekana kwenye runinga, hali isiyoonekana kwa wengine.

Inaelezwa, wanaokuwa wakibanwa sana na wazazi nyumbani wamekuwa wakitoka kwenda kutazama runinga kwa majirani pamoja na kumbi za filamu, maarufu 'vibanda umiza'. Wasiwasi ni, je watoto hupewa vipaumbele kupitia miongozo ya kimaudhui ya filamu hizo?

Mmiliki wa ukumbi wa kuonyesha televishenni wa Sinza, Dar es Salaam ana ufafanuzi wake: "Imekuwa ngumu kwa wengi kuwazuia watoto kwa sababu wengi wao ndio wateja wakuu na hii ni biashara.

"Lakini, hapa kwangu siwezi ruhusu watu wazima pamoja na watoto wachanganyikane wakitizama maudhui ya aibu, huwa nahakikisha nimezipitia kwanza ili nijiridhishe japo wengine hawajali chochote."

## Walimu wanapobeba lawama kuu za kisaikolojia, afya kwa wanafunzi

INATOKA UK.11

"Adhabu kali zitolewe kwa walimu wanaokiuka maadili ya taaluma hii, kwani sisi ni kioo cha jamii na lengo letu ni kujenga taifa lenye vijana wenye nidhamu na maadili mema".

Kihistoria, jukumu la kumjenga mtoto kimaadili ni la jamii, ingawa mzazi au mlezi wanabaki wa kwanza kabisa, wakisimamiwa na usemi "Samaki Mkunje Angali Mbichi"

Kurejea Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, Sura ya 8(1) inatamka "ni wajibu wa mzazi, mlezi au mtu mwingine yeyote anayemlea mtoto kumtunza mtoto huyo.."

Pia, sura hiyo ya sheria ina orodha ya haki za msingi za mtoto, ikijumuisha huduma ya afya na kinga, elimu na muongozo

"Wazazi na walezi ( wakiwamo walimu) wana wajibu wa kuwalea na kuwafundisha watoto katika maadili na mienendo mizuri ya tabia angali bado wadogo, ili waweze kutambua baya na zuri," inafafanua.

Pia, Sura 9 (1) inatamka: "Mtoto atakuwa na haki ya kuishi, utu, heshima, mapumziko, uhuru, huduma za afya, elimu na malazi toka kwa wazazi wake."

Pia, katika kipengele cha tatu kinahanikiza hoja kwa matamshi ya kumlinda mtoto dhidi ya orodha ya mambo kadhaa, ikiwamo; vurugu, unyanyasaji, madhara ya kimwili na kiakili na ukandamizaji, ikitaka kutolewa mwongozo na malezi, msaada na matunzo kwa mtoto na kuhakikisha anaishi kwa kuendelezwa.

AFYA

# Wataalamu: Chanjo inakukwepesha Corona, ikikupata hutalazwa wodini

• Wathibitisha majaribio yalivyofaulu • Utafiti, bingwa chanjo watetea hoja

**Na Mwandishi Wetu**



Shughuli za chanjo nchini Marekani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

"Ni kosa kabisa kufikiria kwamba haina maana katika kupokea dozi za chanjo, kwa sababu kila mtu ataugua tu. Chanjo inafanikiwa katika kubadili kirusi kuwa ugonjwa rahisi, ambao unaweza kutibiwa nyumbani mara nyingi..."

JANGA la maradhi corona limeshika hatua duniani hivi sasa, huku kirusi kipya aina ya omicron ndio kimeshikilia nafasi. Hapo inaongeza utata na maswali, juu ya ubora wa chanjo na inafanya kile kinacholengwa?

Kutoka katika hilo katika baadhi ya nchi kama vile Marekani, Ufaransa, Uingereza na Brazil, zinashuhudia ongezeko la maambukizi kutoka aina mpya za virusi vya delta na ya sasa omicron.

Wanasayansi, madaktari na taasisi za huduma za afya zinaendelea kutegemea aina mbalimbali za chanjo zilizokwishafanyiwa majaribio na kuidhinishwa kimataifa zinafaa kukinga watu na maambukizi.

**UTATA ULIVYO**

Ongezeko la maambukizi katika nchi kama vile Ufaransa na Uingereza, ufanisi wa chanjo kwa mara nyingine tena umerejea kujadiliwa kwenye mitandao ya kijamii.

Baadhi ya watumiaji wa nchi mbalimbali duniani wanakosoa hatua za kiserikali kudhibiti maambukizi kwa chanjo na miongoni mwa malalamiko ni maumivu ya jumla kichwani, mwilini kote, sambamba na uvimbe palikochomwa sindano mtu kujihisi kachoka, baridi na kichefuchefu.

Hata hivyo, wataalamu wa afya wanatetea kazi zao kwamba matukio mabaya kama vile damu kuganda mwilini na majeraha ya moyo (myocarditis) kuwa nadra wakisifu faida za dozi za chanjo ni kubwa kuliko athari zinazoweza kupatikana.

**UFAFANUZI WA BINGWA**

Daktari bingwa wa watoto na magonjwa ya maambukizi nchini Brazil, Renato Kfouri, anafafanua kinachojiri kwenye wimbi la kwanza la chanjo dhidi Covid -19, linalojumuisha chanjo kama za 'Pfizer, AstraZeneca' zikilenga kupunguza hatari ya mtu kuugua sana.

Kwa mujibu wa Dk. Kfouri ambaye pia ni Mkurugenzi wa Shirika la Brazili la Chanjo, ni namna ya ugonjwa wenyewe, kufikia uwezekano wa kulazwa hospitalini na athari zaidi ya hapo.

"Chanjo hulinda vyema mtu dhidi ya kuugua sana na badala yake huumwa kwa kiwango cha kawaida, kidogo au hata kumfanya asipate aina za dalili zozote za Covid," anafafanua.

> **"Ni kosa kabisa kufikiria kwamba haina maana katika kupokea dozi za chanjo, kwa sababu kila mtu ataugua tu. Chanjo inafanikiwa katika kubadili kirusi kuwa ugonjwa rahisi, ambao unaweza kutibiwa nyumbani mara nyingi.**

Anasema lengo hilo la chanjo linadhamiria mbali kuanzia kuzuia maambukizi yenyewe na hatua nyingine ya kulinda mgonjwa asiugue sana, akifafanua: "Lengo hili ni sawa na lengo la chanjo ya mafua ambayo yamekuwapo kwa miongo kadhaa."

Bingwa huyo anasema dozi inayotolewa kila mwaka, siyo lazima izuie maambukizi ya virusi vya mafua, lakini huzuia madhara yake kwa makundi ya watu wanaoweza kuathiriwa zaidi, kama vile watoto, wajawazito na wazee.

Pia, anataja eneo la kuangalia mapana ya ulinzi huo dhidi ya athari za moja kwa moja kwa mfumo wa afya kupunguza maambukizi mabaya ya mfumo wa upumuaji kunakoenda sambamba na idadi ndogo ya wagonjwa katika vyumba vya wagonjwa mahututi.

Takwimu za Jumuiya ya Madola zinaonyesha namna chanjo zinasaidia vyema, ikiwa na ufafanuzi hadi kufikia Novemba 2021 kuna jumla ya vifo milioni 1.1 na watu milioni 10.3 waliolazwa hospitalini nchini Marekani pekee.

Kituo cha Ulaya cha kudhibiti na kuzuia magonjwa (ECDC) na Shirika la Afya Duniani (WHO) kinakadiria watu 470,000 wenye umri wa zaidi ya miaka 60 wamenusurika katika nchi 33 kote barani Ulaya tangu chanjo dhidi ya Covid - 19 ilipoanza kutolewa.

**HALI ILIVYO**

Ni dhahiri kwamba maambukizi ya kujirudia ya mara kwa mara au kupatikana na maambukizi miongoni mwa watu kumeongezeka katika nyakati za hivi karibuni ni hali inayoweza kufafanuliwa kwa njia tatu.



Dk. Renato Kfouri; tabibu bingwa wa Watoto na Magonjwa ya Maambukizi nchini Brazil.

Njia ya kwanza ni rahisi watu wa kawaida waliokusanyika na kusherehekea katika kipindi cha Mwaka mpya na Krismasi, kuongeza hatari ya kusambaa virusi vya corona.

Pili, ni takriban mwaka mmoja baada ya kupatikana chanjo katika baadhi ya maeneo ya dunia, wataalamu waligundua kwamba kinga ya mwili dhidi ya Covid - 19 baada ya kuchanjwa haidumu daima.

"Baada ya muda tumeshuhudia kwamba kiwango cha kinga kinapungua," anatamka Dk. Kfouri, anayeongeza: "Kupungua huku kunaweza kuwa kwa kiwango kikubwa au cha chini kulingana aina ya chanjo na umri wa mtu binafsi."

"Hii inaonyesha haja ya kupata dozi ya tatu, kwanza kwa wazee na wenye kinga ya mwili ya kiwango cha chini, na baadaye kwa watu wote wazima," anafafanua daktari bingwa huyo.

Kigezo cha tatu kinatajwa kuwapo aina mpya ya kirusi omicron kuwa sugu dhidi ya chanjo za awali. Daktari huyo anaendelea: "Kutokana na suala la kwamba watu waliochanjwa hupata maambukizi linapaswa kuangaliwa kama kitu cha kawaida na tutahitajika kujifunza kuishi na hali hii."

"Kwa bahati nzuri ongezeko la hivi karibuni katika maambukizi ya Covid limesababisha kiwango kidogo cha watu wanaolazwa hospitalini na vifo, husussan miongoni mwa watu ambao tayari wamekwishapata chanjo.

"Chanjo inaendelea kuwalinda watu dhidi ya kuugua sana kama ilivyotarajiwa," anahitimisha.

**USHAHIDI WA TAKWIMU**

Chati kutoka Mfumo wa Huduma ya Afya ya New York, inaonyesha ufanisi wa chanjo unaonyesha mwanzoni mwa mwezi uliopita, idadi ya wagonjwa waliolazwa na vifo katika jiji la New York vilipanda kwa kiwango kikubwa miongoni mwa ambao hawakupata chanjo.

Pia, uwasilisho huo wa kitakwimu unaonyesha hakuna mabadiliko miongoni mwa waliochanjwa, wachache kati yao ndio walilazwa na kufariki katika shida ya kiafya inayohusiana na Covid - 19, ikilinganishwa na wasiochanjwa.

**UCHAMBUZI UGHAIBUNI**

Katika ripoti ya hivi karibuni, Shirika la Afya na Usalama la Uingereza, lilifafanua katika majumuishi yanayohusisha Chuo Kikuu cha Cambridge, Uingereza ikionyesha iwapo mtu ataambukizwa kirusi Covid aina ya Omicron, hatari ya kulazwa kwake hospitalini inapungua kwa asilimia 81 na anayechanjwa dozi zote tatu za kinga ya maradhi hayo.

Utafiti mwingine, unaonyesha kwamba chanjo zote tatu zina ufanisi wa asilimia 88, ingawa bado haijafahamika ni muda gani zinadumu na iwapo kutakuwa na haja ya kuchanjwa chanjo nyingine ya kuziboresha katika miezi ijayo.

Mtaalamu bingwa wa masuala ya chanjo, Dk Kfouri, anafafanua ushahidi wote unaoonyesha umuhimu wa kuchanjwa katika dhana ya kukabiliana na aina ya mpya ya virusi omicron.

"Ni kosa kabisa kufikiria kwamba haina maana katika kupokea dozi za chanjo, kwa sababu kila mtu ataugua tu. Chanjo inafanikiwa katika kubadili kirusi kuwa ugonjwa rahisi, ambao unaweza kutibiwa nyumbani mara nyingi.

"Tutatoka katika janga kwa kuchanjwa kwa watu wengi, wakiwamo watoto na heshima kwa huduma za msingi, kama vile kutumia barakoa, kuwazuia watu kuunda umati na kunawa mikono," anahitimisha mtaalamu huyo.

***Kwa mujibu wa BBC***

AFYA

MTAFITI DK. AHMED ALI:

# Dhahabu, manukato na ubani tiba mpya ya saratani, pumu

• Abaini 'zama hizo' zilitumika sana • Mtafiti Mwenza: Uvimbe, meno... • Malighafi toka Somalia yana ziada

**Na Mwandishi Wetu**



Ubani ambao huchomwa kutoa harufu nzuri. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

KATIKA historia ya kiimani huwa kuna vitu vitatu vikuu vyenye thamani kwa binadamu, dhahabu, ubani na manukato.

Sasa kuna hatua zaidi ya kuwapo majaribio ya utafiti wa kitabibu yanayoonyesha kwamba, vitu hivyo vitatu vinaweza kuwa na manufaa katika kutibu maumivu kama vile ya mishipa na pumu na wakati mwingine saratani.

Mwanasayansi wa Chuo Kikuu cha Cardiff nchini Uingereza, Dk. Ahmed Ali, anayefanyia utafiti anasema kuna hatua ya awali aliyobaini, akitazamia kuchunguza ubani na dhahabu kuwa dawa.

"Vitu vyote hivi hutokana na mti unapooza na unaponyauka, ubani huwa donge la dhahabu, huku almasi huonekana kama chembe chembe nyekundu na za rangi ya kahawia,"anaeleza:

Dk. Ali, anatoka nchini Somalia na sasa anaishi Newport, Marekani akitumikia Idara ya Sayansi ya Maisha (bioscience) ya chuo kikuu tajwa, amebeba umaarufu unaomtambulisha kuwa mtambuzi wa ubani, vinavyoweza kutumika kuponya makunyanzi ya mwili pamoja na saratani.

Mtaaluma huyo amegundua ubani wa kwao Somalia, una kemikali tofauti inayofaa kwa ubani wa kawaida na unaweza kutumika kwa tiba nyingi.

"Tumegundua kwamba, unapotoa chembechembe kutoka katika ubani mbalimbali wa Somalia na kuutumia katika kutibu saratani, unafanya kazi ya kuingia ndani ya utendaji wa mfumo mzima wa seli za saratani, kuanzia zilipoanzia hadi zilikosambaa," anaeleza.

Dk, Ali anasema, ni namna inaweza kuzuia kusambaa seli za saratani mwilini. Pia, anataja dhahabu ina manukato, yanayofanyiwa utafiti pia kwa ajili ya matumizi ya tiba ya saratani.

Mtafiti mwenza wake, Profesa Richard Clarkson, anasema utafiti huo unaweza kufikia mafanikio makubwa katika tiba ya saratani.

"Kwa ujumla, lengo ni kupata vitu vipya na dawa ya kuzuia kusambaa zaidi kwa seli za saratani mwilini. Hata hivyo, ni vigumu kutekeleza hata katika kliniki," anasema, huku akiwa na angalizo kuwa ni majaribio ya matibabu yanayochukua muda mrefu, gharama kubwa na anayataja 'ni magumu.'

> **Ubani pia umebainika kuwa unaweza husus an kuzuwia dalili za maambukizi ya utumbo na kuzuia maradhi ya mfumo wa kutoa haja.**

**UNDANI WAKE**

Hadi sasa wanasayansi wamezama katika utafiti kubaini iwapo dhahabu, ubani na manukato ya dhahabu yanaweza kutumiwa kuwa dawa ya tiba.

Profesa Clarkson, ana ufafanuzi kwamba katika maabara, kila kinachoharibu seli zenye afya bila ya madhara, inachukuliwa kuwa yenye manufaa zaidi.

"Unapotafuta kitu fulani kinachofanya kazi kwa kung'amua na kuangamiza seli za saratani na sio kudhuru seli zenye afya, chembe chembe za dhahabu zinaweza kuwa za manufaa sana iwapo utazichanganya na ubani ndani yake," anasema.

"Kihistoria vitu hivi vimekuwa vikichukuliwa kuwa vyenye manufaa sana, kwa hiyo uchunguzi wake unavutia," anafafanua

Dk. Ali anasema alipofanya utafiti, faida nyingine ya ubani aliyoibaini ni kuzuia uvimbe mwilini, akieleza: "Ubani pia umebainika kuwa unaweza kuwa na manufaa katika kutibu ugonjwa wa 'arthritis'.

"Ubani pia umebainika kuwa unaweza hususan kuzuwia dalili za maambukizi ya utumbo na kuzuia maradhi ya mfumo wa kutoa haja."

Hata hivyo, ni utafiti ulioko katika hatua za mwanzo ufafanuzi bado ukibaki wa maabara, licha ya kwamba vitu hivyo vitatu, ubani, dhahabu na ubani vimekuwa vikichukuliwa kama vyenye maana kwa karne nyingi.



Mtafiti Dk. Ahmed Ali.

Mhadhiri wa taaluma ya Historia ya Tiba katika Chuo Kikuu cha Aberisith, Dk. Rachel Gillibrand anaeleza namna alivyoshangaa ubani kuwa katika orodha ya yale yaliyotumiwa zamani kwa ufanisi.

"Ubani haukutumiwa tu kama manukato, bali ulitumiwa katika kutibu magonjwa mengi," anasema.

Dhahabu inatajwa katika historia ya kutibu maumivu ya meno huku kukiwapo zama kwamba watoto walipobainika kuwa na minyoo, walipewa mchanganyiko wa ubani na dhahabu na kunyweshwa kama tiba.

Dk. Gillibrand anasema 'Hippocrates' muasisi wa tiba za kisasa, alipendekeza kutumiwa dhahabu kukabili maumivu ya meno miongo kadhaa katika zama hizo, akiorodhesha ushuhuda kadhaa.

Mojawapo anautaja ni mfupa wa uti wa mgongo wa mwanajeshi Mgiriki uliofukuliwa ulikuwa na ushahidi anaoueleza: "ulituonyesha dhahiri kwamba, wakati ule dhahabu ilitumiwa kwa njia hii...."

**DHAHABU VS SARATANI**

Pasipo ufafanuzi wa kina wa ufundi wake, inaelezwa chembechembe za dhahabu zimetumika katika kutibu kuua seli za saratani katika utaalamu unaoitwa 'radiation therapy' ikirahisishwa 'X-rays' kuingia vyema na kutibu kwa ufanisi zaidi.

Mtaalamu Dk. Gillibrand anafafanua kuwa, pamoja na matumizi hayo, bado nafasi kuu ya ubani na dhahabu imejikita zaidi kiimani kuwa manukato yanayotolewa zawadi.

Mafuta ya dhahabu yalitumiwa katika hadhi ya 'nguo ya kujifunika' na dahabu yenyewe ilichukuliwa kuwa kitu cha thamani tangu zama hizo ikiwa na rangi ya kung'aa, yenye mvuto kwa wengi.

Askofu Gregory Cameron, wa nchini Uingereza anazitaja 'zawadi hizo tatu', pia kwake zina umuhimu kidini..."Kwahiyo manukato yalitolewa kwake kama Masia, ubani ukatolewa kwake kama Kasisi na dhahabu ikatolewa kwake kama Mfalme."

**BIASHARA & MBADALA**

Kwa matabibu asilia 'kidonge' cha ubani kinatajwa kuwa na nafasi ya kutumika kuwa mbadala wa dawa za kumeza kwa kusudi la kuimarisha akili na kumbukumbu, pia kutibu maradhi mengine yanayoendana na ukuaji akili.

Bishara yake imekuwa ikizalishwa kutokana na miti aina ya boswellia inayozalishwa katika mataifa ya Yemen, Omani, Somalia, Ethiopia na sehemu za Bara Hindi inakostawi.

***Kwa mujibu wa taarifa za mtandao***





## Wakulima wafundwa kuhusu akiba chakula

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Maombi na Maombezi kwa Mataifa Yote, Living Mwambapa, amewataka wakulima wa Kanda ya Kati kuweka akiba ya chakula cha kutosha badala ya kukiuza kwa walanguzi ili kuepuka baa la njaa.

Tahadhari hiyo aliitoa jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma na kuwataka kuchukua hatua hiyo ili kujilinda na upungufu wa chakula.

Kutokana na kuchelewa kwa mvua kwa kanda hiyo ya kati na baadhi ya maeneo, alisema wakulima waache kukimbilia kwa walanguzi, badala yake wahifadhi chakula cha kutosha kitakachowezesha kukabiliana na njaa.

Alisema ni vyema wakulima wakajihadhari kwa kujiwekea chakula cha kutosha badala ya kutegemea serikali na wafadhiri kwa ajili ya kusaidiwa.

Katika hatua nyingine, Askofu Mwambapa pia aliwahimiza wakulima kuhakikisha wanatunza chakula walichonacho pamoja na kuwa na nidhamu ya fedha ili kujiwekea akiba ya kutosha ya chakula na mitaji.

"Muda huu mikoa yetu hii ya kanda ya kati unaweza kuona kuwa debe mmoja la mahindi linauzwa Sh. 16,000 na mpaka leo hii mvua haijanyesha na hatujajua mpaka lini itanyesha hivyo tunatakiwa kuliangalia kwa hili," alisema.

Pia aliwataka Watanzania kuendelea na desturi ya kulinda na kutunza amani ya nchi sambamba na kuliombea taifa pamoja na viongozi wake.

**Tahadhari hiyo aliitoa jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma na kuwataka kuchukua hatua hiyo ili kujilinda na upungufu wa chakula.**

# Maelfu kukumbwa magonjwa kisa unene kupita kiasi ifikapo 2030

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TATIZO la unene litakuwa limeenea kwa kiasi kikubwa hususani kwa wanawake na wanaume wenye umri mkubwa ifikapo 2030, imeelezwa.

Dk. Martine Chegere kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alisema hayo wakati wa warsha ya kujadili magonjwa yasioambukiza iliyofanyika jijini hapa chini ya usimamizi wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

Alisema watu wanapaswa kupunguza ulaji wa vitu vyenye sukari ili kujiepusha na tatizo hilo ambalo hutokea baada ya muda mrefu tangu kuanza kutumia vitu vitamu hasa vyenye sukari.

Dk. Chegere alisema kwa mwaka 2014 inakadiriwa kuwa watu bilioni 2.1 walikuwa na uzito mkubwa jambo ambalo halikubaliki.

Nchini Tanzania, alisema kiwango cha kuenea kwa unene kupita kiasi kimeongezeka kwa wanawake na wanaume kutoka asilimia 5.9 mwaka 2014 hadi asilimia 8.4 kwa mwaka 2016.

Alisema unene kupita kiasi kwa hali ya juu ni hatari kupata ugonjwa wa kisukari.

Pia alisema matumizi ya vinywaji vyenye viwango vya juu vya sukari huongeza karoli nyingi mwilini ambazo uhusishwa na kuongezeka kwa uzito uliopitiliza kupita kiasi.

Alisema mazoea ya kutumia vinywaji vilivyonogeshwa sukari wakati wa utoto yanaweza kuendelea katika utu uzima na kuzidisha hatari ya unene kupita kiasi kama hayatadhibitika vema. Daktari huyo alisema tatizo la unene kupita kiasi na magonjwa yasioambukizwa huchangia sehemu kubwa ya mzigo wa magonjwa.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wananchi kuwa makini na masuala ya vyakula ili kuiweka miili yao sawa kiafya ikiwamo kuepuka tatizo la unene kwa binadamu.

Pia aliitaka jamii kuzingatia lishe bora ili kuepuka kupata magonjwa mbalimbali kama kisukari, shinikizo la damu na mengine yanayosababishwa na ulaji ovyo wa vyakula kwa mwanadamu.

Katika warsha hiyo ambayo ilihusisha wataalamu kutoka wizara mbalimbali, COSTECH ilikuwa kwa ajili ya kupokea matokeo ya utafiti mbalimbali uliofanywa na vyuo mbalimbali nchini kuhusiana na magonjwa yasioambukiza na athari zake kwa mwanadamu.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama (katikati), akizungumza na watumishi wa Idara ya Uendelezaji Sera jijini Dodoma jana, wakati wa kikao kazi chenye lengo la kujitambulisha na kutoa mwongozo wa utendaji kazi anaouhitaji. **PICHA: UTUMISHI**

# Viongozi waonywa kuhusu kiburi cha madaraka

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano mkoani Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, amewataka viongozi wake kuwatumikia watu badala ya kujivunia madaraka waliyokabidhiwa.

Pia amewataka kufanya kazi zao kwa kuisaidia serikali pamoja na jamii iliyowazunguka kwa malengo ya kuleta maendeleo pamoja na kudumisha amani na mshikamano.

Dk. Chande alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na viongozi wa Jumuiya ya Maaridhiano waliochaguliwa katika ngazi mbalimbali ikiwamo ya wilaya, kata na vijiji kwenye uchaguzi uliofanyika wilayani humo.

Alisema kuwa viongozi hao wamechaguliwa kwa malengo ya kuwatumikia jamii inayowazunguka na siyo kujivunia madaraka kwa kuwa wakifanya hivyo hawatadumisha amani bali watavuruga na kuhatarisha.

Alisema kuwa serikali kwa upande wake wanahitaji kupata msaada kutoka kwa viongozi hao katika kutoa elimu ya kuimarisha amani na mshikamano ambao umekuwa ukileta maendeleo kwa Watanzania.

"Asilimia kubwa ya Watanzania hawawezi kugombana kwa ajili ya ukabila na udini, hii ni kutokana na amani tuliyonayo, hivyo viongozi ambao mmechaguliwa mnatakiwa kuidumisha na kuilinda amani pamoja na kuwatumikia watu."

Naye Katibu wa Jumuiya ya Maaridhiano Mkoa wa Dodoma, Shabani Shabani, amewataka viongozi hao wa wanaochaguliwa kujiepusha malumbano yasiyokuwa na maendeleo kwa ajili ya masilahi ya Watanzania.

Katibu huyo alisema viongozi wa jumuiya hiyo mmepewa majukumu ya kulinda na kuenzi amani pamoja na kuombea taifa, kuombea amani na mahitaji mbalimbali yanayowagusa Watanzania.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Bahi, Jeremiah Mapogo, akizungumza na viongozi wa jumuiya hiyo ofisini kwake, alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa kwa ajili ya kudumisha amani na mshikamano.

Mapogo alisema kuwa serikali inatambua mchango mkubwa unaoletwa kwa ajili ya wananchi wake kupitia jumuiya hiyo ya Maaridhiano ikiwamo pia kwa upande wa maendeleo.





# Shida maji majimbo sita kumalizwa

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WANANCHI wa majimbo sita ya mkoa wa Mbeya, wanatarajiwa kuondokana na uhaba wa maji ndani ya miezi minane.

Hatua hiyo inatokana na serikali kupitia Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kutia saini mikataba na makandarasi kutekeleza miradi ya maji yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 2.9.

Mikataba hiyo ilitiwa saini juzi katika Ofisi ya Meneja wa RUWASA Mkoa na makandarasi watakaotekeleza miradi hiyo na kushuhudiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Juma Homera.

Kaimu Meneja wa RUWASA Mkoa wa Mbeya, Sambwee Sijabaje, alisema fedha hizo zimetolewa na serikali ili kuwaondolea wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo ambayo wakati mwingine huwa si ya uhakika.

Alisema fedha hizo zitatumika kununua mabomba ya maji na kujenga miundombinu ya maji kuanzia kwenye vyanzo mpaka kwenye makazi ya wananchi wanaolengwa kunufaika nayo.

"Hii miradi ni muhimu, hivyo sisi wasimamizi tunalo jukumu la kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa. Tunawaomba makandarasi muwe waaminifu na mkamilishe miradi kwa wakati," alisema Sijabaje.

Baada ya kutia saini mikataba hiyo, baadhi ya makandarasi waliishukuru serikali kwa kuamua miradi hiyo itekelezwe na makandarasi kwa maelezo kuwa miradi hiyo itasaidia kuongeza ajira kwa wananchi watakaoshiriki kwenye ujenzi.

Mmoja wa makandarasi hao, Johannes Mgosi, alisema miradi mingi ilikuwa inatekelezwa kwa kutumia njia ya akaunti ya dharura (force account), hivyo kuwanyima fursa makandarasi kutekeleza miradi hiyo na hatimaye kukosa fedha.

Aliiomba serikali iendelee kutumia utaratibu huo wa utekelezaji wa miradi kwa kuwa wamewekeza nguvu na rasilimali zao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kama hiyo.

Homera aliishukuru serikali kwa kuidhinisha fedha hizo kwa ajili ya miradi akisema itasaidia kupunguza kero ya maji kwa wananchi wa maeneo ya vijijini hasa kwenye majimbo yaliyopatiwa mgawo.

Alisema mbali na fedha hizo pia kuna miradi mingine ambayo inatekelezwa kwa fedha za semrikali na kwamba mpaka sasa zimefikia Sh. bilioni 8.5.

Alisema fedha za utekelezaji wa miradi hiyo zinatokana na mgawo wa fedha za kukabiliana na madhara ya UVIKO - 19 na zingine ni za miradi ya kawaida ambazo zote zinatolewa na serikali.

"Kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hii, RUWASA hakikisheni mnawatambulisha kwanza makandarasi kwenye majimbo husika ili wafahamike na wananchi wawajue," alisema Homera.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, aliwataka makandarasi hao kutekeleza miradi hiyo kwa uaminifu na kwa kuzingatia muda wa kwenye mikataba.

Alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na wataalamu wataendelea kutembelea miradi hiyo ili kuangalia namna inavyotekelezwa ili kushuhudia kama inatekelezwa kwa mujibu wa makubaliano.



Lori la mizigo likiwa limeziba barabara baada ya kushindwa kupanda mlima na kuanza kurudi nyuma, ambapo liligonga lori lingine la kampuni ya Coca Cola katika mteremko wa Iwambi, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ongezeko kasi gongo latisha

Na Nebart Msokwa, MBEYA

MKOA wa Mbeya unakabiliwa na ongezeko la matumizi ya pombe haramu ya moshi maarufu kwa jina la gongo hali ambayo inahatarisha afya za watu hao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema jeshi hilo limekuwa likifanya operesheni kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo na kuwakamata watu wakitumia ama kuuza.

Kamanda Matei alisema katika operesheni iliyofanyika kuanzia Januari 5, mwaka huu, wameshawakamata watu watatu ambao ni magwiji wa kuuza pombe hiyo haramu kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa na kwamba operesheni hiyo inaendelea.

Alisema Januari 6, makachero wa jeshi hilo walifanya operesheni katika kijiji cha Katumba wilayani Rungwe na kumnasa Atuganile Mwakalobo (52) akiwa na lita 21 za pombe hiyo haramu akiiuza kwa wananchi wa eneo hilo.

Matei alisema mtuhumiwa alikamatwa saa 7:52 mchana akiwa anauza pombe hiyo kwenye kilabu chake cha pombe za kienyeji kilichoko kijijini hapo na kwamba mtuhumiwa ni mzoefu wa biashara hiyo.

Vilevile alisema makachero hao walifanya operesheni katika Wilaya ya Kyela na kumkamata Anyeshi Baton (50) mkazi wa Kijiji cha Kyimo akiwa na lita nne za gongo.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa saa 5:35 asubuhi akiuza pombe hiyo kwenye kilabu chake cha pombe za kienyekji kilichoko katika kijiji hicho cha Kyimo.

"Lakini kumekuwa na tabia ya uingizaji wa pombe zilizopigwa marufuku kutoka nchi jirani, kwenye operesheni tuliyofanya Januari 5 katika Wilaya ya Kyela tulimkamata Gwantwa Mwakajila (45) mkazi wa Ikolo kwa kosa la kuingiza pombe za aina hiyo," alisema Kamanda Matei.

Alizitaja aina ya pombe ambazo mtuhumiwa huyo alikamatwa nazo kuwa ni Ice chupa 20, Carerhum chupa 31, Zikomo chupa 14 ambazo zote zinatoka nchi jirani ya Malawi.

# Utafiti waipa turufu Tanzania ya kuuza mafuta ya kupikia nje

Na Nebart Msokwa, KYELA

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, umebaini kuwa Tanzania itaanza kuuza mafuta ya kupikia nje ya nchi kutokana na ongezeko la eneo linalofaa kwa kilimo cha chikichi na matumizi ya mbegu bora za zao hilo.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema hayo juzi wakati wa ukaguzi wa kitalu cha miche ya zao hilo ambayo imeandaliwa kwa ajili ya kuwagawia wananchi wa Wilaya ya Kyela.

Alisema taasisi hiyo imefanya utafiti kwa kupima udongo ambapo imebaini kuwa yapo maeneo mengi nchini ambayo yanafaa kwa uzalishaji wa zao hilo na endapo fursa hiyo itatumika vizuri kuna uwezekano wa kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta.

Alisema mbali na uwezekano wa Tanzania kuwa na uwezo wa kuuza mafuta nje ya nchi, lakini hata uuzaji wa mazao mengine ya chikichi utaongezeka kwa kiasi kikubwa, hivyo kuliingizia taifa pato kubwa tofauti na ilivyo sasa.

"Tumefanya utafiti wa kubaini maeneo yanayofaa kwa kilimo cha chikichi na kwa wilaya hii tumebaini kuwa maeneo yote yanafaa kwa kilimo cha zao hili, tumeandaa kitalu hiki kwa ajili ya kuwagawia wananchi," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema katika kitalu hicho ambacho wamekiandaa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, kuna miche 15,000 ambayo itagawiwa kwa wakulima wa maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Baadhi ya wakulima wa zao hilo, katika Wilaya ya Kyela, waliiomba serikali iendelee kuwasaidia upatikanaji wa mbegu bora wakidai kuwa miche iliyoandaliwa bado haiwatoshi kulingana na ukubwa wa mashamba yao.

Mmoja wa wakulima hao, Ibrahim Lameck, alisema wananchi wamepatiwa elimu na mbinu za kilimo bora cha zao hilo, hivyo wamehamasika kulima hali ambayo imeongeza hata uhitaji wa mbegu za kisasa.

Alisema endapo watakuwa na uhakika wa mbegu, kuna uwezekano wa kuongeza uzalishaji wa mafuta kama yalivyo malengo la serikali na kwamba itasaidia pia kupunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi.

"Tunaomba uandaaji wa mbegu uwe endelevu maana nina uhakika hii iliyopo haitutoshi kabisa. Tunataka tuondokane na hiki kilimo chetu cha kienyeji ambacho tija yake ni ndogo," alisema Lameck.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Kyela, Benard Libata, alisema kutokana na ushirikiano uliopo kati ya halmashauri na TARI, wananchi wana uhakika wa kupata mbegu bora za michikichi na kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji.

Alisema wataendelea kushirikiana na taasisi hiyo ili kuhakikisha wanaliendeleza zao hilo ambalo lilikuwa linapuuzwa kutokana na tija kuwa ndogo.

Naye Mratibu wa Chikichi kutoka TARI Uyole, Beatha Paul, alisema endapo miche hiyo itapandwa kwa kufuata taratibu za kitaalamu itatosha kupandwa kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 700.

Alisema kutokana na miche hiyo kuwa tayari kupandwa, wanaendelea na utaratibu wa kuwahamasisha wananchi kulima zao hilo ili kufikia malengo yanayotakiwa.



HABARI ZANZIBAR

# Shein pekee atunukiwa nishani ya Mapinduzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein, ni kiongozi pekee kwa mwaka huu aliyetunukiwa nishani ya Mapinduzi ikiwa ni kielelezo cha kuyatukuza na kuyaenzi Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Nishani hiyo alitunukiwa nishani hiyo juzi na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, katika hafla iliyofanyika katika viwanja vya Ikulu, Zanzibar na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali.

Rais Dk. Mwinyi kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 10(1) na 2 cha Sheria ya Mambo ya Rais Na. 3 ya mwaka 2020 na kama ilivyotangazwa katika tangazo la kisheria namba 24 la mwaka 2022 kupitia gazeti rasmi la serikali, ametunuku nishani moja ya Mapinduzi kwa kiongozi huyo mstaafu.

Akisoma wasifu wa Dk. Shein, Kapteni Martin Mabena alisema Rais mstaafu Dk. Shein alizaliwa Machi 13, 1948 huko Chokocho Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba. Mwaka 1956 alianza masomo ya msingi katika Skuli ya Msingi ya Wanafunzi wa Kiume ya Gulioni wakati huo ikiitwa Gulioni Boy's Primary School Zanzibar.

Mwaka 1965 hadi 1968, alipata masomo ya sekondari katika Chuo cha Lumumba Zanzibar na Dk. Shein alianza masomo ya sekondari ya juu mwaka 1969 na kukamilisha mwaka 1970 katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Vorenezh iliyokuwa Urusi.

Kapteni Mabena alisema Dk. ni daktari kitaaluma, aliyehitimu katika fani ya baiokemia ya utabibu kutoka Chuo Kikuu cha Odessa, Russia kati ya mwaka 1970 na 1975. Mwaka 1984 hadi 1988 alipata shahada ya uzamivu (PhD) ya fani kemikia na magonjwa ya binadamu katika Chuo Kikuu cha Newcastle, Uingereza.

Alisema kati ya mwaka 1981 na 1994 alihudhuria programu mbalimbali za mafunzo, zilizofanyika ndani na nje ya nchi, zikiwamo huduma za utoaji damu na uendeshaji wa benki za damu yaliyofanyika Stockholm , Sweden na mwaka 1994 alipata mafunzo ya Uongozi (management and situation leadership), Dar es Salaam.

Mwaka huo huo alishiriki mafunzo ya masuala ya kupambana na VVU/Ukimwi katika nchi zinazoendelea katika Chuo Kikuu cha East Anglia, Norwich nchini Uingereza.

Aliongeza kuwa Dk. Shein alianza kazi ya ukarani katika Wizara ya Elimu Zanzibar Mei, 1969 na baadaye mwaka huo huo alipangiwa kazi ya Katibu Mkuu Msaidizi 'B' wa wizara hiyo hiyo hadi Septemba 1969 alipoondoka kwenda USSR.

Kati ya mwaka 1979 na 1984 alikuwa Mkuu wa Idara ya Huduma za Maabara ya Patholojia, Wizara ya Afya Zanzibar. Aliporejea kutoka masomo ya PhD mwaka 1989, aliteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Patholojia katika Wizara ya Afya Zanzibar na alitumikia hadi mwaka 1991.

Aliteuliwa kuwa Meneja Programu wa Mpango wa Kudhibiti Ukimwi Zanzibar ndani ya Wizara ya Afya na Mshauri wa Kliniki ya Biokemia na Huduma za Uchunguzi kati ya 1991 na 1995.

Maisha yake ya kisiasa yalianza pale alipowania kiti cha Baraza la Wawakilishi kupitia Jimbo la Mkanyageni kisiwani Pemba katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1995. Oktoba 29, 1995 aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Afya wa Zanzibar Novemba 13, mwaka huo.

Novemba 20, 2000 aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais anayeshughulikia Katiba na Utawala Bora.

Dk. Shein aliteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania Julai 13, 2001. Mwaka 2005 aliteuliwa kuwa mgombea mwenza wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na hatimaye kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania na kuapishwa Desemba 21, 2005. Aligombea urais wa Zanzibar mwaka 2010 na kuchaguliwa kuwa Rais Oktoba 31, mwaka huo. Aliapishwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Novemba 3, 2010.

Katika shughuli zake za kitaaluma, Dk. Shein amechapisha tasnifu za utafiti mbili, ambazo ni tasnifu ya utafiti alioufanya wakati akikamilisha masomo ya shahada ya uzamili na tasnifu ya utafiti alioufanya wakati akikamilisha masomo ya shahada ya uzamivu. Aidha, amefanikiwa kuchapisha nyaraka mbalimbali za kitaalam. Dk. Shein aliwahi kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

Pia Dk. Shein ameteuliwa na Rais wa Tanzania kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Januari, jana. Amewahi kuwa mwanachama wa vyama kadhaa vya kitaalamu. Kwa sasa Dk. Shein ameoa na ana mke na watoto.

## Waliokosa ajira wapewa tumaini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Hamid Seif Said, amewataka wananchi waliokosa ajira katika awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya huko Pangatupu, kuwa wastaamilivu kwa kuwa kuna fursa zaidi za ajili katika mradi huo.

Alisema fursa hizo zinatoka kwa awamu kulingana na maendeleo ya mradi, hivyo akwataka wananchi kustamili na kuahidi kushirikana na msimamizi wa mradi kwa kuhakikisha anatoa kipaumbele cha ajira kwa wananchi wanaoishi karibu na eneo la mradi.

Akizungumza na baadhi ya wananchi waliofika kijiji cha Pangatupu kwa lengo la kutafuta ajira, ujio wao umeonyesha wazi kuwa na moyo na utayari wa kushirikiana na serikali yao katika miradi ya maendeleo.

Alisema serikali imeamua kujenga hospitali hiyo kwa lengo la kusogeza karibu huduma ya afya kwa wananchi na kuondokana na tatizo la kuifata huduma hiyo katika masafa marefu.

Hata hivyo, mkuu huyo wa wilaya aliitaka kampuni inayosimamia mradi huo kuongeza bidii ili kukamilisha ujenzi huo kwa wakati na kiwango kilicho bora.

Msimamizi wa mradi kutoka kampuni ya World Class Engineering, Egespo Mbuligwe, alisema hospitali hiyo ya ghorofa moja inatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi sita.



Wafuasi wa vyama vya ACT-Wazalendo na CCM, wakiwa katika maandamano wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi Zanzibar, katika Uwanja wa Amaan jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri asisitiza dhamira ya elimu bure

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema serikali imedhamiria kuendeleza sera ya elimu bure kwa kila mwananchi bila ya ubaguzi wowote.

Alisema hayo juzi wakati akizindua kongamano la kuadhimisha miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar, lililofanyika katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kampasi ya Maruhubi mjini Zanzibar.

Haroun alisema matukio ya uzinduzi wa miradi ya maendeleo inayoendelea kuzinduliwa na viongozi wa kitaifa ikiwamo miradi ya elimu inadhihirisha wazi kuwa Zanzibar inapiga hatua za maendeleo.

Alisema serikali imedhamiria kuleta maendeleo makubwa kwa kufanya mageuzi ya kiuchumi kupitia uchumi wa bluu ili Zanzibar kukua kiuchumi kupitia rasilimali za bahari.

Endapo rasilimali za bahari zitatumiwa kwa weledi na ufanisi, alisema zitastawisha huduma za kijamii zikiwamo afya, elimu, barabara, maji na michezo.

Alitumia fursa hiyo kuwataka wanafunzi wa chuo hicho kujifunza kwa bidii ili Zanzibar kupata wataalamu wa kutosha ambao watasaidia katika utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu na mipango ya maendeleo na mafanikio ya kiuchumi yanaletwa na wataalamu wa ndani.

Naye Rais wa Serikali ya Wanafunzi (SUZASO), Sleyum Abdallah Ali, alisema katika kuadhimisha miaka 58 ya Mapinduzi, vijana wengi walipata fursa ya kushiriki katika shughuli za maendeleo ikiwamo ufunguzi wa miradi, maandamano na matembezi.

Pia alisema kupitia klabu za mazingira, usafi ulifanyika katika maeneo mbalimbali pamoja na utoaji wa elimu ya UVIKO- 19 kwa wananchi.

Alisema serikali ya wanafunzi itaendelea kuenzi, kuthamini na kudumisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa kuwa uwapo wa chuo hicho ni miongoni mwa matunda ya Mapinduzi.

HABARI PICHA

# SHEREHE YA MAADHIMISHO YA MIAKA 58 YA MAPINDUZI MATUKUFU YA ZANZIBAR



Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea Wimbo wa Taifa, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Amaan Zanzibar jana, kwa ajili ya kuhudhuria sherehe za Maadhimisho ya Miaka 58 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. PICHA ZOTE: IKULU



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwapungia mkono wananchi, wakati alipowasili katika Uwanja wa Amaan kwa ajili ya kuhudhuria sherehe hizo.



Waandamanaji vijana wakipita na picha za marais wa Zanzibar tokea enzi za mapinduzi



Kikosi cha Kutuliza Ghasia cha Jeshi la Polisi (FFU) wakila kiapo cha utii mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani) wakati wa sherehe hizo.



Askari wa Kikosi cha Makomando wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ), wakionyesho umahiri wao katika sherehe hizo.



Sehemu ya viongozi mbalimbali na wananchi waliohudhuria sherehe hizo.

**HABARI KIMATAIFA**

## Bomu uwanja wa ndege laua wanane Somalia

**Mogadishu,** SOMALIA

TAKRIBANI watu wanane, wameuawa katika mlipuko wa bomu katika mji mkuu wa Somalia, Mogadishu, waokoaji wamesema. Kundi la wapiganaji wa Kiislamu la al-Shabab, limesema lilitekeleza shambulio hilo.

Mlipuko huo, ulitokea kwenye barabara ya eneo la kuingia kambi ya Jeshi la Wanaanga la Somalia, ambalo iko karibu na uwanja wa ndege wa kimataifa.

Walioshuhudia tukio hilo, wameliambia shirika la habari la AFP kwamba, msafara wa usalama wa kibinafsi, ukiwasindikiza wageni, ulikuwa ukipita wakati bomu hilo likilipuka.

"Mlipuko huo ulikuwa mkubwa kiasi kwamba umeharibu majengo mengi yaliyo karibu na barabara na magari yanayopita eneo hilo," Hassan Nur alisema.

Kundi la wanamgambo wa Kiislamu la Al Shabab, mara kwa mara hutekeleza mashambulizi ya kujitoa mhanga.

Somalia pia, iko katikati ya mzozo wa kisiasa kutokana na mzozo wa madaraka kati ya rais na waziri mkuu, kabla ya uchaguzi. **BBC**

## Aliyenadi mabati ya nyumba kulipa mateka achangiwa

**Lagos,** NIGERIA

SAIDU Faskari, amepokea mamia ya maelfu ya Naira baada ya kujaribu kuuza paa la nyumba yake, ili kupata pesa za kukomboa zilizodaiwa na watekaji nyara wa mtoto wake wa kiume mwenye umri wa miaka 17.

Faskari, mwenye umri wa miaka 65, ambaye yeye mwenyewe pia alitekwa nyara Desemba, mwaka jana, Kaskazini-Magharibi mwa Jimbo la Katsina na aliachiliwa baada ya mtoto wake kuwalipa watekaji nyara dola 121, Alhamisi iliyopita.

Hata hivyo watekaji nyara walimkamata mtoto huyo na kumwachilia baba yake.

Faskari, aliambiwa kuchangisha dola 242, kwa ajili ya kumkomboa mtoto wake.

Video iliyoonyesha akishusha paa la nyumba yake, ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii baada ya kuchapishwa kwenye Facebook na majirani zake.

Haijajulikana ni kiasi gani kilikuwa kimekusanywa kufikia juzi, lakini Faskari alisema watu wanapaswa kuacha kutuma pesa kwa sababu lengo limefikiwa.

Vitendo vya utekaji nyara ili kulipa fidia, limeenea Nigeria huku watekaji nyara wakidai chochote kuanzia dola 50 hadi dola milioni moja. **BBC**

# Shambulizi la ndege isiyo rubani laua 19

**Tigray,** ETHIOPIA

WATU 19 wameripotiwa kuuawa katika mashambulizi ya ndege zisizoruka na rubani katika mkoa wa Tigray Kaskazini mwa Ethiopia.

Mashuhuda wamesema watu kadhaa walijeruhiwa katika shambulizi hilo, duru kutoka eneo hilo, zimesema wahanga wote walikuwa raia.

Iliarifiwa kuwa shambulizi hilo, lilikipiga kiwanda cha kusaga unga katika mji wa May Tsebri, Kusini mwa Jimbo la Tigray.

Hiyo ni hujuma ya hivi karibuni ya shambulizi la ndege isiyoruka na rubani, linakuja siku chache tu baada ya shambulizi kama hilo kuilenga kambi moja ya wakimbizi wa ndani.

Shambulizi la Ijumaa wiki iliyopita, liliwaua watu wasiopungua 59 na kuwajeruhi karibu 140.

Umoja wa Mataifa (UN), ulisema hauwezi kuthibitisha kwa njia huru shambulizi la karibuni, kwa sababu njia za kuingia eneo hilo zimefungwa.

Serikali ya Ethiopia pia ilisema haina taarifa kuhusu tukio hilo.

**DW**



Maofisa usalama Somalia, wakikagua eneo lilikolipuka bomu eneo la Hamarweyne, mjini Mogadishu, na kuua takribani watu wanane, jana. **PICHA: REUTERS**

## Vikwazo Mali vyaligawa Baraza la Usalama UN

**New York,** MAREKANI

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa, lilikutana wiki hii kuhusu hali ya Mali na wajumbe katika mkutano huo waligawanyika kuhusiana na vikwazo vilivyochukuliwa dhidi ya nchi hiyo ya Afrika.

Nchi za Afrika na Ufaransa, zilitaka baraza hilo kukutana ili kupitisha msimamo wa pamoja kuelekea jeshi lililo madarakani nchini Mali.

Na kwamba jumuiya ya kimataifa inaunga mkono Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), ambayo ilichukuwa vikwazo vipya dhidi ya Bamako, baada ya utawala wa kijeshi kupinga kufanyika kwa uchaguzi kama ilivyoahidiwa.

Urusi na China zilizuia rasimu ya tamko hilo.

Katika mkutano huo, mwakilishi wa UN nchini Mali alitoa taarifa kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na kuwakumbusha wanachama 15, kuhusu mazingira ambayo mashauriano ya kitaifa yalifanyika na hitimisho lao, tangazo la mamlaka ya mpito kuahirisha uchaguzi wa rais hadi mwisho wa mwaka wa 2026.

Majibu ya ECOWAS na vikwazo vilitangazwa siku chache baadaye.

Kwa upande wake, mwakilishi huyo, anaona kuwa Braza la Usalama la Umoja wa Mataifa, litaendelea kufanya kazi pamoja na mamlaka ya Mali, ECOWAS na Umoja wa Afrika, AU, ili kuondokana na mkwamo huo.

Walinda amani 1,000 wa ziada wa Chad, waliokubaliwa na Bamako, wanapaswa kuwezesha hali ya mambo kubadilika.

Umoja wa Mataifa na wajumbe wa Baraza, wamelalamika kuhusu kuzorota kwa hali ya usalama nchini Mali, wakikumbusha walinda amani 28, waliouawa mwaka jana, aliripoti mwandishi wa RFI, New York, Carrie Nooten. **RFI**

## Urusi, NATO yaijadili Ukraine

**Brussels,** UJERUMANI

MAOFISA wa ngazi za juu wa Jumuiya ya Kujihami (NATO) pamoja na wa Urusi, wamekutana mjini Brussels, katika juhudi za kupunguza tofauti baina ya pande hizo kuhusu mustakabali wa Ukraine.

Mazungumzo hayo yamefanyika jana, kukiwa na mashaka makubwa, kuhusu uhalisia wa mapendekezo ya Rais wa Urusi, Vladimir Putin, juu ya usalama wa nchi yake.

Mkutano huo wa Brussels ni mmoja katika mfululizo wa mingine inayofanyika wiki hii, chini ya jitihada za Marekani kuepusha mvutano ambao nchi za Magharibi zinaamini unaweza kuishia katika uvamizi wa Urusi dhidi ya Ukraine.

Urusi mara zote imekanusha kuwa na nia ya kufanya shambulio hilo.

Ujumbe wa Urusi katika mkutano huo unaongozwa na manaibu waziri wake wa mambo ya nje, Alexander Grushko na wa ulinzi Alexander Fomin.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Wendy Sherman, atakuwapo pia katika makao makuu ya NATO kuhudhuria mkutano huo. **DW**

# JULIO: NAMUNGO FC TUTAREKEBISHA ULINZI

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio' (pichani) amesema michuano ya Mapinduzi imewapa mwanga na kuongeza kitu kwenye kikosi hicho ili kiwe tishio kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Julio alisema baada ya kuona mapungufu yaliyojitokeza katika michuano hiyo, tayari wameanza kufanyia kazi ikiwemo safu ya ulinzi.**

Alisema mchezo wao wa nusu fainali dhidi ya Simba umewapa mwanga mzuri wa kuona jinsi gani kikosi chao kinatakiwa kufanyiwa kazi sehemu ya ulinzi.

"Kwa siku mbili hizi tutakaa na Kocha Mkuu, Honor Janza kufanyia kazi mapungufu yetu kabla ya kuwavaa Polisi Tanzania katika mchezo wetu wa Ligi Kuu," alisema Julio.Alisema malengo makubwa kwa sasa ni kuimarisha kikosi cha timu hiyo kuwa imara na bora kwa ajili ya kurejea kwenye ligi kuu.

"Tunahitaji kufanya vizuri katika michezo ya ligi kuu, malengo yetu ni kuhakikisha tunapambana kutafuta matokeo kila mechi ili kuwa miongoni mwa timu zitakazokwenda kuwakilisha nchini michuano ya kimataifa," alisema Julio.

Alisema ana imani hilo linawezekana kwa sababu kuna mambo madogo wanayafanyia kazi kuhakikisha timu yao inakuwa tishio katika michezo iliyopo mbele yao ikiwemo dhidi ya Polisi Tanzania.

Namungo baada ya kuondolewa hatua ya nusu fainali ya Mapinduzi imerejea jijini Dar es Salaam leo na inatarajia kuelekea Moshi kwa ajili ya mchezo dhidi ya Polisi utakaopigwa Januari 17, 2022, uwanja wa Ushirika, Kilimanjaro.





Viongozi wa bendi ya Tukuyu Sound, Kalala Junior (kulia) na Papii Kocha wakifanya vitu vyao kwenye onyesho la bendi hiyo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Geita Gold yatikisa usajili dirisha dogo*

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali isiyo ya kawaida, klabu ya Geita Gold imeweka rekodi ya kusajili wachezaji wengi kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufungwa Jumamosi ya Januari 15.

Geita Gold imezipiku klabu kubwa za Simba, Yanga na Azam kwa idadi ya wachezaji iliyosajili, achilia mbali timu zingine za Ligi Kuu, huku ikiwa ni timu mpya na inayocheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza msimu huu.

Tayari imesajili wachezaji saba, tena baadhi wakiwa wenye majina makubwa kwenye Ligi Kuu, wakiwa wametoka au kuwahi kuzichezea klabu kubwa nchini.

Wachezaji iliyowasajili ni William Gallas, ambaye chimbuko lake ni kikosi cha pili cha Simba na kupandishwa kikosi cha kwanza 2012, lakini pia ikimsajili straika kutoka Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo, Erick Yema.

Geita Gold pia, imepata saini ya wachezaji wawili waliotokea kwenye klabu ya Yanga, Adeiyum Suleiman na Ditram Nchimbi, lakini pia ikimsainisha beki wa zamani wa klabu ya Simba, Mbeya City na Kagera Sugar, Juma Nyosso.

Beki wa zamani wa klabu za Simba na Yanga, Kelvin Yondani naye amekula mkataba wa mwaka mmoja kwenye klabu hiyo, lakini Aron Kalambo, kipa wa zamani wa Prisons naye pia amesajiliwa na timu hiyo.

Klabu ya Yanga nayo ni moja kati ya timu iliyolitumia vizuri dirisha la usajili, kwani imesajili wachezaji wanne, ambao ni Denis Nkane kutoka Biashara United, Salum Aboubakar kutoka Azam, Crispin Ngushi kutoka Mbeya Kwanza na Aboutwalib Mshery kutoka Mtibwa Sugar.

## Michuano ya FA Zanzibar kuanza Januari 15

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MICHUANO ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (FA CUP) inatarajia kuanza kutimua vumbi Januari 15 , 2022.

Michuano hiyo inacheza kwa Kanda mbili za Unguja na Pemba kwa mujibu wa kanuni ya Mashindano hayo msimu huu 2021-2022.

Kanda ya Unguja kutakuwa na jumla ya timu 38 ambapo 12 za ligi kuu zilizopo Unguja, 16 za ligi daraja la kwanza Kanda ya Unguja na 9 kutoka mikoa mitatu ya Unguja.

Kwa upande wa Kanda ya Pemba itakuwa na timu 34 ambapo timu nne za ligi kuu ya Zanzibar zilizopo kisiwani Pemba, timu 24 za ligi daraja la kwanza kanda ya Pemba na timu sita kutoka mikoa miwili ya Pemba.

Kwa mujibu wa kanuni ya Mashindano mshindi wa michuano hiyo kwa kanda ya Pemba atacheza na mshindi wa kanda ya Unguja ili kupata timu itakayoiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la shirikisho Barani Africa, CAF.

## Kiiza atatupia sana Bongo - Baraza

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, amesema kuwa straika Hamisi Kiiza ni mzoefu kwenye Ligi Kuu ya Tanzania Bara, hivyo ana uhakika kuwa ataisaidia timu hiyo kwa kufunga mabao, kitu ambacho kinawaangusha kwa sasa.

Akizungumza baada ya klabu hiyo kutangaza kumsajili straika huyo wa zamani wa Simba na Yanga, raia wa Uganda, amesema kuwa kwenye kikosi chake ana wachezaji wazuri wenye uwezo wa kukaa na mpira kwa muda mrefu, lakini kinachokosekana ni kuweka mpira ndani ya wavu.

"Ni wachezaji wazuri, wana uwezo wa kukaa na mpira kwa muda mrefu, wanamiliki mpira, lakini tatizo ni kwenye umaliziaji, nina washambuliaji lakini bado ni vijana na wanahitaji mtu mmoja mkongwe na mzoefu ili kuwafanya na wao wajifunze kitu," alisema Baraza ambaye ni raia wa Kenya.

Kuhusu umri wa mchezaji huyo, Baraza alisema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara au soka kwa ujumla, tatizo huwa si umri bali uwezo wa mtu.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### HATIMA YA HAALAND

KLABU ya Borussia Dortmund inatazamiwa kukutana na mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland, 21, wiki ijayo huku wakijaribu kujua mipango ya mchezaji huyo kuhusu mustakabali wake. ***(Marca)***

### SEVILLA WAMTOSA MARTIAL

SEVILLA wametuliza nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial, 26, kwa vile hawawezi kumudu matakwa ya Manchester United ya kumsajili kwa mkopo mchezaji huyo. ***(Marca)***

### HAITAKI NEWCASTLE

KIUNGO wa Paris St-Germain, Georginio Wijnaldum, 31, amekuwa akihusishwa na Newcastle United, lakini mchezaji huyo hana nia ya kurejea katika klabu hiyo yake ya zamani. ***(Football Insider)***

### MOURINHO AMTAKA NDOMBELE

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho amewasiliana na kiungo wa kati, Tanguy Ndombele, 25, katika juhudi za kumshawishi kiungo huyo wa kati wa Ufaransa ajiunge naye katika klabu ya Roma, huku klabu hiyo ya Italia ikitaka mkataba wa mkopo na chaguo la kumnunua. ***(Telefoot, via Mail)***

### RASHFORD NA MKATABA MPYA

MSHAMBULIAJI wa England, Marcus Rashford, 24, anatarajiwa kufanya mazungumzo na Manchester United kuhusu mkataba mpya. ***(Mail)***

### NKETIAH KUTUA PALACE

KLABU ya Crystal Palace ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa England, Eddie Nketiah, 22, kutoka Arsenal, huku mkataba wa mchezaji huyo ukimalizika msimu wa joto. ***(Times)***

### ATAKIWA MIDDLESBROUGH

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa vijana wa Arsenal na timu ya taifa ya England, Folarin Balogun, 20, anatazamiwa kujiunga na Middlesbrough kwa mkopo kwa muda wote uliosalia wa msimu huu. ***(Sky Sports)***

### SENESI AGOMBEWA

KLABU za Brighton na Newcastle United zinapanga kujaribu kumsajili beki wa Argentina, Marcos Senesi, 24, kutoka klabu ya Uholanzi ya Feyenoord. ***(Football Insider)***


### EKITIKE AWANIWA

KLABU za Brentford na Brighton zimewasilisha ombi la kutaka kumsajili mshambuliaji wa Reims, Hugo Ekitike, 19, lakini Newcastle United ndio wanapewa nafasi kubwa ya kumsajili Mfaransa huyo. ***(90 Min)***

### SPURS KUSAJILI BEKI

TOTTENHAM Hotspur inataka kumsajili beki wa kulia, wakati huu wa dirisha dogo la usajili Januari, baada ya mkutano kati ya kocha, Antonio Conte, Mwenyekiti Daniel Levy na Mkurugenzi Mkuu wa Soka Fabio Paratici. ***(Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TUCHEL AMHAKIKISHIA NAFASI LUKAKU

**Asema ni suala la muda tu, atakuwa namba 9 wa kudumu na...**

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amesema Romelu Lukaku anahitaji muda kuweza kuzoea mahitaji ya nguvu kwenye Ligi Kuu England, lakini amesisitiza hatajaribu kumuacha tena straika huyo.

**Straika huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alirudi pale Stamford Bridge alikosajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Inter Milan Agosti mwaka jana.**

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 bado hajarudi kwenye ubora wake katika kipindi hiki cha pili kucheza pale Blues, akifunga mabao nane kwenye mechi 20 alizoichezea kwenye mashindano yote.

Lukaku hivi karibuni aliachwa na Tuchel baada ya kutoa kauli ya kusema kwamba, "sina furaha na hali ilivyo" na kujikuta akiwa kwenye wakati mgumu, wakati alipobainisha kwamba, ana mpango wa kurudi kwa Nerazzurri siku moja.

Hata hivyo, straika huyo aliomba radhi kwa kocha na mashabiki, na alirudi kuanza kwenye kikosi cha kwanza wiki iliyopita katika nusu fainali ya kwanza ya michuano ya Carabao waliyoshinda dhidi ya Tottenham.

Na Tuchel anaamini kwamba, ni suala la muda tu kumfanya straika huyo kuwa namba 9 wa kudumu.

Alisema: "Romelu alikuwa na mchango mkubwa wa nguvu kwenye mchezo dhidi ya Tottenham.

"Pengine hakuhusika sana, lakini alionesha kiwango cha kuvutia na ubora wa hali ya juu.

"Mara atakapoweza kuzoea staili ya uchezaji kwenye Ligi Kuu, hakuna shaka kwamba atakuwa na mchango mkubwa zaidi."

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 846

MECHI KALI

LIVERPOOL
VERSUS
ARSENAL

1 | 2.00
X | 3.60
2 | 3.35

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# VILLA YAKAMILISHA USAJILI WA COUTINHO



**LONDON,** England

ASTON Villa imekamilisha usajili wa Philippe Coutinho kutoka Barcelona kwa mkopo na atacheza hapo hadi mwisho wa msimu huu.

Villa ilitangaza Ijumaa iliyopita kwamba imefikia makubaliano ya kumsajili mchezaji huyo pale Villa Park.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 29 aliwasili jijini Birmingham Jumanne, na sasa klabu imethibitisha dili hilo limekamilika.

Coutinho alisema: "Najisikia furaha kuwa hapa hii ni klabu kubwa.

"Nimezungumza mengi na kocha na ameniambia kuhusu klabu na matarajio yake. Nina furaha kubwa kuwa hapa na nasubiria kufurahia soka.

"Nasubiri kukutana na mashabiki, kuwa uwanjani. Najua kwamba nina furaha kwa sababu nipo hapa.

"Nataka kulipa fadhila uwanjani na kufurahia soka. Nasubiria kwa hamu kuwa uwanjani.

"Mara zote nataka kuwa kwenye ubora wangu, kufanya kazi yangu. Hiyo ndio sababu najituma kwa bidii kila siku. Natumaini nitakuwa na kipindi kizuri cha msimu kilichobaki hapa."

Coutinho, ambaye anavaa jezi namba 23, alitumia miaka mitano akiwa anacheza kule Liverpool kati ya mwaka 2013 na 2018.



## Salah azungumzia hatima yake

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah amesisitiza halazimishi kupewa mkataba "mnono sana" wakati akirudia kusema kwamba, majaliwa yake Liverpool yapo mkononi mwa klabu hiyo.

Nyota huyo wa Misri mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni msimu wa 2022-23 na bado hakujawa na mazungumzo yoyote kuhusu kuuongeza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 awali alisema kwamba anataka kubakia Anfield, lakini ni juu ya Wekundu hao wanaomilikiwa na kampuni ya Fenway Sports Group kufikia makubalino.

Akizungumza na GQ, Salah alisema klabu inataki wa kuonesha thamani yak kwa mafanikio aliyoipa kla bu hiyo tangu alipotua hap akitokea AS Roma mwak 2017.

"Nataka kubaki, lakini hil halipo kwenye mikono yan gu. Lipo mikononi mwao, alisema. "Wanajua nini nin achokitaka. Sijasema natak mkataba mnono sana."

,297,200

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/01/22 | 18:00 | Mallorca vs Espanyol | 2.50 | 2.94 | 2.99 |
| 02. 15/01/22 | 18:15 | OH Leuven vs Mechelen | 2.31 | 3.49 | 2.81 |
| 03. 15/01/22 | 18:30 | Boavista vs Gil Vicente | 2.87 | 3.12 | 2.46 |
| 04. 15/01/22 | 20:30 | Monchengladbach vs Bayer Leverkusen | 2.54 | 3.69 | 2.49 |
| 05. 15/01/22 | 20:30 | Sporting Gijon vs Cadiz CF | 2.50 | 2.99 | 2.94 |
| 06. 15/01/22 | 20:30 | Girona vs Rayo Vallecano | 2.52 | 3.11 | 2.81 |
| 07. 15/01/22 | 20:45 | NEC Nijmegen vs Heracles Almelo | 2.35 | 3.29 | 2.85 |
| 08. 15/01/22 | 21:00 | Nancy vs Bastia | 2.70 | 3.09 | 2.60 |
| 09. 15/01/22 | 21:00 | US Quevilly Rouen vs Amiens | 2.81 | 3.20 | 2.43 |
| 10. 15/01/22 | 23:30 | Betis vs Sevilla FC | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 11. 16/01/22 | 16:30 | Cambuur vs Sparta Rotterdam | 2.37 | 3.49 | 2.70 |
| 12. 16/01/22 | 17:00 | Lorient vs Angers | 2.37 | 3.19 | 3.04 |
| 13. 16/01/22 | 18:00 | Eupen vs Cercle Brugge | 2.95 | 3.35 | 2.28 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 13/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 5748 | Arema vs PSS Sleman | 1.86 | 3.33 | 3.81 |
| 14:30 | 2333 | MES Rafsanjan vs Peykan FC | 2.14 | 2.90 | 3.48 |
| 14:30 | 3208 | Teraktor Sazi vs Nassaji Mazandaran | 2.50 | 2.93 | 2.79 |
| 14:30 | 3866 | Aluminium Arak vs Sepahan Esfahan | 3.86 | 2.94 | 2.00 |
| 14:30 | 5521 | Havadar vs Sanat Naft Abadan | 2.34 | 2.79 | 3.18 |
| 14:30 | 5907 | Zob Ahan vs Gol Gohar | 2.71 | 2.81 | 2.66 |
| 15:00 | 1623 | Naft Masjed Soleyman FC vs Esteghlal Tehran | 6.35 | 3.46 | 1.53 |
| 15:30 | 5299 | AL Faiha vs Al Fateh (KSA) | 2.30 | 3.28 | 3.03 |
| 16:00 | 3808 | Niki Volou vs AO Trikala | 1.54 | 3.57 | 5.79 |
| 16:20 | 1996 | Al Gharafa SC vs Lekhwiya SC | 4.53 | 4.34 | 1.54 |
| 16:20 | 4255 | Al-Sailiya SC vs Al Arabi Doha SC | 2.90 | 3.52 | 2.12 |
| 16:30 | 1409 | Foolad Khuzestan vs Padideh Mashhad | 1.46 | 3.66 | 6.94 |
| 16:45 | 2600 | Persib Bandung vs Bali Utd Pusam | 2.50 | 3.03 | 2.70 |
| 17:00 | 1988 | Chennaiyin FC vs Hyderabad FC | 3.52 | 3.56 | 1.87 |
| 17:00 | 4474 | Persepolis FC vs Fajr Sepasi | 1.21 | 5.03 | 13.54 |
| 17:45 | 3345 | Al Hidd Club vs Muharraq SC | 4.23 | 3.42 | 1.75 |
| 19:00 | 3697 | AL Wakrah vs Al Khoor | 1.69 | 3.76 | 4.15 |
| 19:00 | 4318 | Cameroon vs Ethiopia | 1.20 | 5.55 | 17.84 |
| 19:15 | 2671 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs AS Tel Aviv University W | 2.60 | 3.42 | 2.36 |
| 20:00 | 4123 | Napoli vs Fiorentina | 1.78 | 3.78 | 4.03 |
| 20:15 | 5546 | Maccabi Bnot Emek Hefer W vs Bnot Netanya W | 1.13 | 7.73 | 11.60 |
| 20:20 | 4798 | Al Ahli Manama vs Al Hala Muharraq | 2.27 | 3.18 | 2.89 |
| 20:45 | 2464 | Hapoel Raanana W vs MS Kiryat Gat W | 14.43 | 7.89 | 1.11 |
| 21:00 | 2950 | Bourg Peronnas vs Bastia Borgo | 1.56 | 3.92 | 5.30 |
| 21:00 | 3451 | Famalicao vs Belenenses | 1.65 | 3.65 | 5.13 |
| 21:00 | 3635 | Hapoel Hadera vs Bnei Sakhnin | 2.29 | 3.27 | 2.79 |
| 22:00 | 3944 | Atletico Madrid vs Athletic Bilbao | 1.92 | 3.25 | 4.04 |
| 22:00 | 5959 | Cape Verde vs Burkina Faso | 3.52 | 2.93 | 2.25 |
| 22:00 | 5980 | Hapoel Marmorek Rehovot W vs Hapoel Beer Sheva W | 2.12 | 3.71 | 2.79 |
| 22:30 | 1072 | Lecce vs Vicenza | 1.34 | 4.79 | 8.02 |
| 22:30 | 3060 | Benevento vs Monza | 2.10 | 3.25 | 3.39 |
| 22:45 | 1295 | Liverpool vs Arsenal | 2.00 | 3.60 | 3.35 |
| 23:00 | 3660 | AC Milan vs Genoa | 1.30 | 5.13 | 8.88 |
| 23:00 | 4137 | CSD Arzua vs SD Juvenil de Ponteareas | 1.62 | 3.85 | 4.52 |
| 23:45 | 5435 | Portimonense vs Mafra | 1.60 | 3.72 | 4.83 |

### IJUMAA - 14/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 02:00 | 3044 | Tepatitlan FC vs Correcaminos Uat | 1.70 | 3.48 | 4.45 |
| 11:15 | 3934 | Persik Kediri vs PS Tni | 2.70 | 3.22 | 2.39 |
| 12:00 | 3707 | Menemen Belediye Spor U19 vs Bandirmaspor U19 | 3.95 | 3.65 | 1.88 |
| 14:00 | 4009 | FC Vizela U23 vs Vitoria Guimaraes U23 | 1.98 | 3.76 | 3.03 |
| 14:15 | 1725 | Persepam MU vs Bhayangkara Surabaya Utd | 4.72 | 3.47 | 1.67 |
| 14:15 | 4710 | Barito Putera vs Pusamania Borneo | 4.81 | 3.75 | 1.60 |
| 15:15 | 5416 | AL Akhaa AL Ahli vs Al-Nejmeh | 12.48 | 5.57 | 1.19 |
| 15:35 | 5958 | Al Raed Club vs Al Ittihad Jeddah | 3.86 | 3.81 | 1.82 |
| 15:50 | 2308 | Abha vs AL Baten | 1.93 | 3.67 | 3.57 |
| 16:00 | 1208 | Hapoel Afula vs Hapoel Ramat Gan | 2.53 | 3.18 | 2.78 |
| 16:00 | 1827 | Senegal vs Guinea | 1.75 | 3.27 | 5.15 |
| 16:00 | 4468 | Sectzya Nes Ziona vs Hapoel Acre | 2.17 | 3.21 | 3.36 |
| 16:00 | 5578 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Rishon Lezion | 2.06 | 3.37 | 3.47 |
| 16:00 | 5810 | Hapoel Raanana vs Hapoel Petah Tikva | 2.65 | 3.00 | 2.85 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KMC YAIFUATA PRISONS KIBABE

**Na Dennis Fussi**

TIMU ya KMC inaondoka Dar es Salaam leo kuelekea mkoani Rukwa kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Prisons, utakaopigwa Jumapili kwenye Uwanja wa Nelson Mandela.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari na Mawasiliano wa KMC, Christina Mwagala, kikosi hicho kinaondoka na wachezaji 23 pamoja na viongozi wa benchi la ufundi ambapo wamejipanga kuhakikisha wanapata pointi zote tatu.

KMC Januari 6 ilimtambulisha, Thierry Hitimana kuwa kocha wake mkuu akichukua nafasi ya John Simkoko pamoja na msaidizi wake, Habibu Kondo pia itakuwa na mchezo mwingine wa Ligi Kuu dhidi ya Mbeya Kwanza utakaopigwa Januari 21.

"Tunaenda kucheza mechi mbili ugenini ambazo kimsingi zitakuwa ngumu, tunakocha mkuu mwingine, ambaye ameanza kukinoa kikosi hicho hivi karibuni, hivyo tumejipanga kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema Mwagala.

Aidha, alisema timu imekuwa na wakati mzuri wa mazoezi kuelekea mchezo huo na kwa upande wa hali zao ni nzuri, kwani wana morali kubwa ambayo kimsingi inajenga ari ya kwenda kupambana.

"Malengo yetu ni kupata matokeo mazuri ikiwa katika mapambano ya mkakati wa kujiimarisha katika msimamo wa Ligi kuu, ili tuweze kujinasua kutoka kwenye nafasi ya 12 tuliyopo sasa."



Miongoni mwa wabunifu watakaoshiriki katika onyesho la Safari Fashion Week kutoka kushoto, Mustafa Hassanali, Jamila Vera Swai na Martin Kadinda linalotarajiwa kufanyika Januari 28 hadi 30 mwaka huu, katika hoteli ya Mawemawe iliyoko mkoani Manyara. **PICHA: MTANDANO**

# Ney wa Mitego hataki kusifia sifia

**Na Sabato Kasika**

RAPA wa Hip Hop, Ney wa Mitego amesema, hana mpango wa kuimba nyimbo za kusifia sifia au za mapenzi, badala yake ataendelea kujikita katika nyimbo zinazoelimisha mambo mbalimbali yakiwamo ya kijamii na kisiasa.

Msanii huyo aliyeachia wimbo mpya wa 'Hunijui' mwishoni mwa Desemba mwaka jana, amesema hayo alipokuwa akizungumza na gazeti hili, jijini Dar es es Salaam jana kuhusu msimamo wake katika muziki.

"Binafsi huwa sibabaishwi na maneno ya watu wanaodai kuwa ninashambulia wengine kupitia muziki wangu, lakini ukweli ni kwamba nyimbo zangu zinaelimisha na nitaendelea kufanya hivyo," amesema Ney wa Mitego, ambaye jina lake halisi ni Emmanuel Elibariki.

Ney wa Mitego, amesema, anajua nyimbo zake nyingi ambazo amekuwa akitoa, huwa zinawaudhi watu wengi hasa wasiopenda kuambiwa ukweli, na kwamba hilo halimfanyi aogope kusema ukweli alionao

"Kwanza ni lazima tuelewane kwamba, mimi ni msanii sipangiwi cha kuimba, kwani ninatoa kile ambacho ni hisia zangu ili kufikisha kwa jamii, hivyo siogopi mtu awe kiongozi awe nani nitamchana tu," amesema.

Msanii huyo ambaye amekuwa akitamba na nyimbo mbalimbali zikiwamo za Shika Adabu yako Niwachane na nyingine nyingi, amesema wale ambao wamekuwa wakimzungumza vibaya hawamjui.

"Upo wimbo wangu unaitwa Acha Niongee ambao umewahi kuzua gumzo mtandaoni, kutokana na ukweli ninaoimba, wale wanaojua kile ninachoimba, wanapenda sana nyimbo zangu, wasioelewa nitaendelea kuwachana," amesema.

# Michezo

Alhamisi Januari 13, 2022

**Nipashe**




**Tuchel amhakikishia nafasi Lukaku** UKURASA 21



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini. **PICHA: SIMBA**

# *Fainali ya akili*

## ●●● Pablo wa Simba asema wachezaji wake wapo kamili gado, huku Azam watamba kulibebe taji la...

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

UBINGWA wa Mapinduzi ndio neno limekuwa likitajwa na makocha wa timu mbili za Simba, Pablo Franco na Azam FC, Abdihamid Moallin kuelekea fainali ya kombe la Mapinduzi leo.

**Mchezo huo utakaopigwa katika uwanja wa Amaan, Visiwani Unguja ni fainali ya pili kwa timu hizo kukutana katika mashindano hayo, mara ya kwanza ikiwa mwaka 2019.**

Katika mchezo huo, Azam FC walitwaa ubingwa kwa ushindi wa 2-1 dhidi ya Simba, katika dimba la Migombani Pemba, mabao yakifungwa na Mudathir Yahya na Obren Chirwa na Shiza Kichuya kwa wekundu wa msimbazi.

Mchezo wa leo utakuwa wa ushindani mkubwa ikiwa kila mmoja malengo yake kuhitaji kuondoka na kombe la Mapinduzi. Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo alisema mikakati yao ni kuhakikisha wanafanya vizuri kila michuano na mwaka 2022 wanaanza na kombe la Mapinduzi.

Alisema wamejiandaa vizuri, wachezaji wako fiti na tayari kwa ajili ya kupambana kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kulibeba taji hilo.

"Wachezaji walicheza kwa kiwango bora sana dhidi ya Namungo FC, nina matarajio makubwa kwa mchezo wa kesho (leo), utakuwa mzuri na ushindani mkubwa kwa wenzetu na kwetu pia ,"



Baadhi ya wachezaji wa Azam FC. **PICHA: AZAM**

"Azam ina wachezaji wazuri na wanapambana kutafuta matokeo, tumeona ubora wao na kuufanyia kazi, tuna waheshimu, tutacheza kwa tahadhari ili kufikia malengo yanayotarajiwa wa wana Simba wote,"alisema Pablo.

Kwa upande wa kocha wa Azam, Moallin alisema wamefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo na anaamini utakuwa wa ushindani mkubwa.

Alisema amewaona wapinzani wao hao, wataingia kwa nidhamu ya hali ya juu kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kutwaa ubingwa wa Mapinduzi.

"Utakuwa mchezo wa ushindani, tunaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri ili kufikia malengo yetu, Simba ni timu nzuri lakini tunaenda kucheza kwa tahadhari kubwa ili kupata ushindi," alisema Moallin.

# Yanga yawapeleka Ninja, Kibwana kutibiwa Tunisia

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imewapeleka wachezaji wake wawili, Kibwana Shomari na Abdallah Shaibu 'Ninja' nchini Tunisia kwa matibabu.

Taarifa rasmi ilitolewa jana mchana na klabu hiyo kwenye mtandao wake wa instagram, ikiwataarifu wanachama, mashabiki, wapenzi na wadau wengine wa soka kuwa, imeamua kuwapeleka nchini humo ili kufanyiwa matibabu kutokana na majeraha waliyoyapata kwenye mechi mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Klabu ya Yanga imewapeleka wachezaji wake wawili, Kibwana Shomari na Abdallah Shaibu nchini Tunisia kufanyiwa matibabu kutokana na majeraha waliyoyapata. Pia wachezaji wetu wameambatana na daktari wa viungo Youssef Mohamed." Klabu hiyo iliandika taarifa yake hiyo kwenye mtandao rasmi wa klabu.

Kibwana na Ninja wamekosekana kwenye mechi kadhaa za Ligi Kuu kwenye klabu hiyo pamoja na mechi za Kombe la Mapinduzi.

Kibwana, ambaye anacheza beki ya kulia na kushoto, ndiye anayeonekana kukosekana kwake kumekuwa pengo kwenye klabu hiyo na kuonekana hata kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi kiasi cha kuvuliwa ubingwa.

Watakuwa ni wachezaji wa tatu sasa kupelekewa nje ya nchi kutibiwa. Mwezi Novemba mwaka jana, Yanga ilimpeleka nchini humo mchezaji wake raia wa Burkina Faso, Yacouba Songne na kufanyiwa upasuaji wa goti.

Kwa sasa mchezaji huyo anauguza jeraha hilo, ambalo kwa mujibu wa madaktari anatakiwa kukaa nje miezi mitano ili aanze tena mazoezi mepesi.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, SL P 9